# Nipashe

Ijumaa Oktoba 16, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580370

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**WAUAWA** usiku kwa madai ya mgogoro kugombea shamba

UKURASA 2



**MAALIM** Seif azuiwa kampeni kwa siku 5


UKURASA 7




**Courtois amtabiria makubwa Hazard**

UKURASA 22

# Dk. Shoo afunguka



• **Akemea** udhalilishaji wagombea, asema viongozi wa dini kuegemea vyama ni kuwagawa waumini...*Endelea ukurasa 2*

## Tundu Lissu atanabaisha atakuwa rais Katiba Mpya

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Waliokufa kwa maji Dar sasa wafikia 12

UKURASA 2


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

HABARI KITAIFA

# Dk. Shoo akemea udhalilishaji wagombea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amekemea vitendo vya kupigwa na kudhalilishwa kwa baadhi ya wagombea hasa wanawake katika kampeni za uchaguzi na kutahadharisha kuwa iwapo vitendo hivyo, vitaachiwa viendelee vitahatarisha amani.

Sambamba na hilo, amesema suala la viongozi wa dini kuegemea chama kimoja cha siasa linapaswa kukemewa kwa kuwa linawagawa wananchi.

Askofu Dk. Shoo aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mdahalo wa viongozi wa dini kuhusu kuhamasisha ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na ngazi za uamuzi.

Mdahalo huo umeandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake (UN-Women).

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kutoegemea upande mmoja kwa kuwa watu wa vyama vyote ni waumini wao.

"Unapoegemea waziwazi chama kimoja, tukijua hawa ni wanasiasa na siasa ni mchezo wa aina yake, kama viongozi wa dini, maandiko yanaelekeza vizuri kabisa namna ya kusimama na namna ya kuhitaji wote kuwashauri na kuwaombea alisema. Kuhusu vitendo vya udhalilishaji, Dk. Shoo alisema lugha za kudhalilisha zinamkwamisha mwanamke kushiriki kwenye uongozi hivyo zinapaswa kukemewa. "Tumekemea na kutahadharisha kwamba uvunjifu wa amani unaanza na jambo dogo kwa hiyo si tu wanawake, kuwadhalilisha, kuwapiga wagombea wa aina yoyote hususan wanawake. Linapotokea jambo la namna hiyo, linagusa hisia za watu. Nasema mambo hayo ni ya kukemewa na kuachwa mara moja na jamii yetu," alisema.

"Tumeshuhudia lugha za udhalilishaji hasa kipindi hiki cha kampeni. Ni vyema mdahalo ukatoka na tamko la kukemea wale wote wenye lugha za udhalilishaji wanawake," alisisitiza.

Alisema pia suala la rushwa linamkwamisha mwanamke licha ya kuwa na uwezo.

"Hii imesababisha wanawake kushindwa kuthubutu kujitokeza kushiriki kwenye ngazi za maamuzi, sisi viongozi wa dini tunapaswa kulaani na kukemea vitendo hivi viovu, wanawake wanayo haki ya kushika nafasi,"alisema.

Hata hivyo, alisema wanawake wanaojitambua hawapaswi kuwa na hofu zinapozungumziwa haki za wanawake.

Dk. Shoo alisema kuna ushiriki duni wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi, ambapo ngazi ya ubunge wanawake ni asilimia 36.9, ambao wanatokana na majimbo na viti maalum.

Alitaja mambo manne, ambayo viongozi wa dini wanapaswa kusimamia ni kuhamasisha ushirikishwaji wa wanawake katika ngazi za uongozi na uamuzi, kuzuia migogoro isiyo ya lazima, kejeli, lugha za kashfa na udhalilishaji hususan kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi.

"Wale tunaofahamu nafasi ya mama sawasawa hakuna kinachoudhi unaposikia mtu anakutukania mama yako au anamdhalilisha mama. Ni kitu kinagusa hisia, tuchunge ndimi ni muhimu sana," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakari Kunenge, akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, wakati akitangaza vifo vya watu 12, vilivyotokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa inayonyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliokufa kwa maji Dar sasa wafikia 12

**Na Romana Mallya**

WAKATI mvua zikiendelea kunyesha jijini Dar es Salaam, idadi ya vifo imeongezeka na kufikia 12, baada ya wengine wanne waliosombwa na maji kuokotwa Mto Msimbazi.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa, miongoni mwa waliofariki dunia ni watoto wawili wa familia moja, ambao nyumba yao ilikumbwa na mafurikio eneo la Kigogo Buyuni.

Alisema watoto hao, ambao ni Hussein Awadhi (5) na Bakari Awadhi (14), walisombwa na mafuriko baada ya nyumba yao kujaa maji.

Alisema Ibrahimu Hassan (24), mkazi wa Kigogo Buyuni wakati akijaribu kumwokoa mmoja wa watoto hao, naye alisombwa na kupoteza maisha.

Mambosasa alimtaja mtu mwingine kuwa ni mwanamume anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 30 na 35, kukutwa maeneo ya Mabibo mwili wake ukielea kwenye mfereji unaopeleka maji Mto Msimbazi.

Aliwataja wengine waliofariki tangu mvua hizo zianze jijini humo kuwa ni Mariam Yahaya (45), mkazi wa Vingunguti ambaye alikufa wakati akiokoa vyombo vyake visisombwe na maji na mwili wake kukutwa Mto Msimbazi.

"Wengine ni Herieth Kanuti (18), mwanafunzi wa kidato cha tatu, Shule ya Sekondari Lutihinda na Ipyana Mwakifuna (19), mkazi wa Jangwani ambaye ni mgambo, wote vifo vyao viliripotiwa siku ya Jumanne," alisema.

Alisema juzi Philip Felician (30), mkazi wa Tabata Kimanga, mwili wake ulikutwa umenasa kwenye matope katika Mto Tenge baada ya kudondoka na kusombwa na maji wakati akijaribu kuvuka kwenye daraja la waenda kwa miguu huko Tabata.

Alisema mwanaume mwingine anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 30 na 35 alikutwa amefariki dunia katika eneo la Ukonga Sabasaba, mji mpya.

Kamanda Mambosasa alitaja majina ya familia ya watu watano iliyopoteza maisha juzi baada ya moto kutokea kwenye nyumba yao huko Pugu, kuwa ni Jackline Frank (27), mwanafunzi wa Pugu Sekondari.

Wengine ni Esther Katemi (15), mwanafunzi wa Pugu Sekondari, Edward Katemi (11), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Pugu, Edson Katemi (10), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Green Hill na Ivon Katemi (4).

Alisema chanzo cha moto huo ni hitilafu ya umeme iliyoanzia kwenye swichi ya nyumba hiyo.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, alisema zaidi ya nyumba 800 zimeathiriwa na mvua hizo.

Kunenge alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya mvua zinazoendelea kunyesha kwa kuhakikisha wanafuatilia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

# Wauawa madai mgogoro shamba

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WATU wawili wameuawa kwa kushambuliwa na watu wasiojulikana katika mtaa wa Mafisa kwa Mambi, Manispaa ya Morogoro huku chanzo cha mauaji hayo kikidaiwa mgogoro wa shamba.

Mauaji ya watu hao yalitokea usiku wa kuamkia jana yakidaiwa kuwa yametokana na mgogoro wa shamba katika kijiji cha Kisaki wilayani Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa tayari jeshi hilo linamshikilia Rajabu Hamisi (26) mkazi wa Msamvu Ndege Wengi, Manispaa ya Morogoro.

"Ni kweli tukio hilo lipo na huyo mtuhumiwa tumeshamkamata na tunaendelea kumhoji. Upelelezi ukikamilika hatua za kisheria zitachukuliwa," alisema Mutafungwa.

Aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Bernadetha Kibwana anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 60 na 665 mkazi wa kijji cha Kisaki, ambaye inadaiwa alikuwa ndiye mlengwa katika tukio hilo na Zaibabu Maulid mkazi wa Mafisa kwa Mambi, ambaye anadaiwa alikuwa akijaribu kutoa msaada.

Kamanda alisema tukio hilo lilitokea nyumbani kwa Martha Mkude, ambako alikuwa akiishi kwa muda na Kibwana, ambaye inadaiwa alikuwa akisubiria kesi yake ya shamba katika Mahakama ya Ardhi. Kesi hiyo ilipangwa kutajwa Oktoba 29, mwaka huu.

Mkude, mmliki wa nyumba aliyokuwa akiishi Kibwana, alisema watu wasiojulikana walianza kuvamia nyumba za jirani kwa lengo la kumtafuta bibi huyo na walipofika katika chumba alichukuwa amelala, walianza kumshambulia.

Alisema baada ya watu hao kufanikisha mauaji ya mama huyo ndipo alipojitokeza jirani yake, Maulidi kwa lengo la kumsaidia, bila mafanikio kisha naye kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani.

Naye Athumani Bakari, ni mjukuu wa Kibwana, alisema bibi yake alikuja mjini kwa lengo la kumtibia mjukuu wake mwingine, ambaye ni mlemavu wa viungo baada ya kupigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kuwa ni msamaria mwema anataka kuwasaidia.

Alisema baada ya kufika, bibi huyo alianza kumtilia shaka msamaria huyo kutokana maswali yake, ndipo alipoamua kumpigia simu mjukuu wake kuondoka na kwenda nyumbani na Martha kwa ajili ya kusubiria kesi yake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mafisa kwa Mambi, Ahmed Salum, alisema baada ya kupata taarifa kwa majirani kuhusu tukio hilo, alifikisha taarifa polisi na kwamba hatua mbalimbali zimechukuliwa, ikiwamo kumkamata mtuhumiwa.

# Tundu Lissu: Nitakuwa Rais wa katiba mpya

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA Urais (CHADEMA), Tundu Lissu, amewaomba wananchi wa Kanda ya Ziwa kumchagua katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, akiahidi kuiongoza nchi kwa kufuata katiba mpya itakayopatikana.

Amesema nchi inahitaji katiba hiyo kwa sasa, ili kurudisha mamlaka kwa wananchi kujichagulia viongozi kwenye maeneo yao na kuwawajibisha wanapokosea.

Lissu aliyasema hayo jana akiwa katika mikutano ya kampeni wilayani Rorya mkoani Mara na Busega mkoani Simiyu.

"Ninataka niweke wazi, mimi nikuwa rais aina ya Nyerere. Kwanini? Kwa sababu Mwalimu Nyerere mwaka 1978 alikuwa anahojiwa na BBC kuhusu mamlaka yake, alisema hivi; 'kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi, mimi ninaweza kuwa na mamlaka ya kuwa dikteta'.

"Mimi nitakuwa rais wa katiba mpya. Nchi hii inahitaji katiba mpya na katiba mpya ni mkataba wa wananchi, kurudisha mamlaka ya wananchi," alisema.

Lissu alisema katiba hiyo itarudisha mamlaka kwa wananchi kwa kuwawezesha kuchagua viongozi wao, wakiwamo wakurugenzi wa miji, majiji, wakuu wa mikoa na wilaya.

Katika mikutano yake hiyo ya kampeni, Lissu pia aliwaombea kura madiwani na wabunge wa majimbo katika kanda hiyo, akiwamo Ezekiah Wenje anayegombea ubunge wa Rorya.

"Hapa tupate mtu jasiri katika eneo la Rorya, kura ya pili mumpe Ezekiah Wenje, kura yako wa tatu ninaomba mnipigie niwe rais wa nchi hii. Tuchague madiwani, kazi ya diwani na mbunge ni kukutetea wewe na siyo kuitumikia serikali," alisema.

Lissu alisema mfumo wa kodi hautakuwa wa kukusanya kodi kwenye maeneo yao na kuzipeleka hazina, badala yake zitabaki maeneo zinakokusanywa.

"Rais ndiyo kila kitu, ni katiba hii imempa mamlaka yote, tunahitaji katiba mpya ndugu zangu, nitakuwa rais atakayeleta katiba mpya, muundo mpya wa utawala, nitakuwa rais na mfariji mkuu," alitamba.

Lissu pia alisema akipata urais, atabadili mfumo wa elimu ili kuwa na mfumo utaojenga maarifa kwa wananchi ili waajirike katika soko la ndani na nje ya nchi.

"Watoto wetu watapata ujuzi, tutafumua mfumo wa elimu, siyo tu watapata elimu bora, bali tutafungua mipaka ili waende nchi zingine za wenzetu, hata ukitaka kwenda Afrika Kusini, nenda," alisema.

Kuhusu sekta ya afya, Lissu alisema serikali yake itahakikisha kila Mtanzania anajiunga na mfumo wa matibabu kwa kutumia bima ya afya, ili kuwapunguzia gharama za matibabu wananchi.

"Ukienda hospitali sasa kabla hujatibiwa unalipia, wanaougua wakiwa na bima, wakienda hospitali hakuna haja ya kulipa pesa." alisema.

Alisema wananchi wakishaichagua CHADEMA, watakuwa na uhakika wa kupata uhuru na haki ya kulima, kuuza mazao na kuvua samaki bila bugudha.

■**Imeandikwa na Christina Mwakangale na Frank Maxmillian (TUDARCo)**

**TANPORT PUBLIC LIMITED COMPANY**
**P. O. Box 78710**
**DAR ES SALAAM – TANZANIA**

**SHERIA YA KAMPUNI [CAP 212 R.E 2002]**
**MAAUMIZI YA KUFUNGA KAMPUNI YA UMMA YA TANPORT**

*(Imepitishwa Chini ya kifungo Namba 334 cha Sheria za Kampuni [SURA YA 212 R.E. 2002]*

**Kwamba, KAMPUNI YA UMMA YA TANPORT** ni Kampuni ya Umma iliyosajiliwa chini ya Sheria za Kampuni [SURA YA 212 R.E 2002] yenye ofisi zake Plot No 43 - Block Kurasini, Barabara ya Bandari 1 - Dar es Salaam.

**Kwamba** mnamo **tarehe 29 Septemba 2020** Wanachama wa Kampuni hiyo waliamua kwa **UAMUZI MAALUMU** kwamba kampuni inayojulikana kama **KAMPUNI YA UMMA YA TANPORT** ifungwe kwa hiari.

**SASA HIVYO MAAMUZI MAALUMU YAMEAMUA KAMA IFUATAVYO:**

1. **IMEAMULIWA KUWA:** Kampuni inayojulikana kama KAMPUNI YA UMMA YA TANPORT ifungwe kwa hiari.
2. **IMEAMULIWA KUWA:** Kampuni ilikomesha shughuli zake tangu tarehe 29 Septemba 2020.
3. **IMEAMULIWA KUWA:** Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni sasa inajishughulisha na kusuluhisha mambo ya kampuni kwa madhumuni ya kuwezesha mchakato wa kuifunga kampuni kulingana na kama ilivyoainishwa chini ya vifungo 333 na 338 ya Sheria ya Kampuni [Sura ya 212 RE 2002].
4. **IMEAMULIWA KUWA: BW. VICTOR MREMA** atakuwa Mfilisi kwa kusudi la kuifunga kampuni na usambazaji wa mali za Kampuni. Anwani yake kwa ajili ya ya mashauriano / maswali yoyote ni:

**VICTOR MREMA – Wakili**
B & E Ako Law
Nyumba No 7 | Plot 30
Ursino Street | Regent Estate | Mikocheni
SLP 71748 | Dar es Salaam | Tanzania
Simu ya mkononi: + 255 784 424 146
Simu ya mezani: + 255 22 277 1145
Barua pepe: victor.mrema@beakolaw.co.tz

**Imepitishwa Dar es Salaam siku hii ya 9 ya Oktoba 2020**

215946202




Sheikh Mkuu wa Tanzania Abubakari Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, akiwataka Watanzania kudumisha amani katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu mwezi huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbaroni wakituhumiwa kubaka mtoto kwa zamu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linawashikilia vijana wawili, wakazi wa mkoani hapa kwa tuhuma za kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka sita kwa zamu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 12, mwaka huu majira ya saa tatu kasorobo usiku.

Alisema watuhumiwa hao (majina yao yanahifadhiwa kutokana na kuwa na umri chini ya miaka 18), walimlaghai mtoto huyo kuwa watamnunulia pipi pamoja na kumpatia hela, na kisha kumpeleka vichakani nyuma ya nyumba yao na kuanza kumbaka kwa zamu. "Tukio la kubakwa kwa mtoto huyu liligunduliwa na mama yake mzazi (jina limehifadhiwa), ambaye alikuwa akimtafuta mwanawe na kumuona akiwa ameumia sehemu za siri, ndipo akatoa taarifa polisi," alisema Magiligimba.

Alisema chanzo cha mtoto huyo kubakwa ni tamaa za kingono na kwamba upelelezi ukikamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani, ili kuchukuliwa hatua kali zaidi za kisheria.

Pia, kamanda alitoa wito kwa wazazi na walezi mkoani humo, kuendelea kutoa taarifa za ukatili, ili wahusika wachukuliwe hatua na kukomesha vitendo hivyo.

**TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC**
P. O. Box 3010, Arusha Telephone: +255 27 2544872,
Fax: +255 27 254 8213, Email: info@tfa.co.tz

The Tanganyika Farmers' Association PLC
TFA
Since 1935

**ILANI YA MKUTANO MKUU WA MWAKA**

**ILANI INATOLEWA** kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Tanganyika Farmers' Association PLC utafanyika katika viwanja vya TFA Arusha Shopping Centre vilivyopo barabara ya Sokoine, eneo la Ngarenaro Mjini Arusha siku ya Jumamosi tarehe 07 Novemba 2020 mnamo saa nne asubuhi (04:00) kwa madhumuni yafuatayo:-

1. Kufungua Mkutano Mkuu.
2. Kusoma Ilani ya kuitisha Mkutano Mkuu.
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika Arusha tarehe 30/03/2019.
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 30/03/2019.
5. Taarifa ya Mwenyekiti.
6. Kupokea na kupitisha taarifa ya kifedha iliyokaguliwa kwa Mwaka wa fedha ulioishia 2018/2019, pamoja na taarifa ya Wakurugenzi na Wakaguzi wa mahesabu.
7. Kuzingatia kwamba wakaguzi wa nje wataendelea kukagua mahesabu kwa mujibu wa kifungu cha 170(2) cha sheria ya makampuni.
8. Kuidhinisha malipo ya Wakurugenzi kwa Mwaka unaofuata.
9. Mapendekezo ya kuuza magari ya Kampuni.
10. Shughuli nyingine yeyote ile pale ambapo taarifa inayostahiki itakuwa imepokelewa.
11. Kufunga Mkutano Mkuu.

Kwa Amri ya Bodi ya Wakurugenzi

Pendo Jacob
**KATIBU WA KAMPUNI**
16/10/2020

**ELEZO:** Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye Matawi yote ya TFA na kwenye tovuti www.tfa.co.tz

21594502

# WaterAid yasaidia shule mapambano kipindupindu

**Na Beatrice Shayo,** KISARAWE

SHIRIKA lisilo la kiserikali la WaterAid Tanzania, limetoa msaada wa mashine za kunawia mikono kwa wanafunzi zenye thamani ya Sh. milioni 19 ili kujikinga na magonjwa ya milipuko kikiwamo kipindupindu.

Msaada huo umetolewa kwa shule mbili za msingi ya Chanzige A na Chanzige B zilizoko Wilaya ya Kisarawe, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Unawaji Mikono Duniani.

Akizungumza katika maadhimisho hayo jana, Mkurugenzi Mkazi wa WaterAid, Anna Mzinga, alisema wanatambua umuhimu wa siku ya kunawa mkono na kuamua kuadhimisha pamoja na wanafunzi wa shule hizo kwa kuwapatia msaada.

"Tumetoa hivi vifaa vya kunawa mkono pamoja na elimu tuliyowapatia bado kuna haja ya kuwafundisha watoto wetu umuhimu wa kunawa na maji tiririka kwani ni kinga ya kuambukiza magonjwa ikiwamo kipindupindu," alisema.

Alisema hata ugonjwa wa corona walifanikiwa kupambana nao kutokana na unawaji wa mkono, hivyo wanaunga na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika unawaji wa mkono itasaidia kuwapo na afya salama.

"Kampeni hii inalenga uboreshaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira ikiwapo na msisitizo mkubwa katika ubadilishaji wa tabia kwa jamii na kuzipokea tabia zinazoshauriwa na wataalam ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji na sabuni," alisema.

Mzinga alisema pasipo huduma sahihi za maji na usafi wa mazingira katika makazi yetu, shule, vituo vya kutolea huduma za afya na taasisi zingine, mazingira yatakuwa vyanzo vya magonjwa na kuacha jamii ikiwa katika hatari ya kupata milipuko ya magonjwa ya kuambukiza.

Alisema Siku ya Unawaji Mikono Duniani ilianzishwa kwa lengo la kuongeza ufahamu kwa jamii juu ya umuhimu wa kunawa mikono kwa maji na sabuni. Kaulimbiu ya mwaka huu kidunia inasema 'Usafi wa Mikono kwa Wote' ikiwa ni wito kwa watu wote kufanya suala la usafi wa mikono liwe ni tabia ya kawaida na ya kudumu.

Naye Katibu Twala wa Wilaya ya Kisarawe, Mwanana Uwesu, alisema elimu hiyo itawasaidia wanafunzi hao kujikinga na maradhi mbalimbali na kuwa na afya bora pamoja na kuhudhuria shuleni kwa wingi.

Aliwataka wananchi kuweka vifaa vya kunawa mikono katika maeneo yao ili kujikinga na magonjwa.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi, Salehe Segumba, alishukuru kwa msaada waliopatiwa na kwamba itawasaidia wanafunzi kujiepusha na magonjwa yatokanayo na uchafu.

# M'biashara matatani madai kuingiza sukari ya magendo

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kigoma, linamshikilia mfanyabiashara anayedaiwa kuingiza sukari na mafuta nchini, kimagendo na kufanya udanganyifu wa kufunga upya kwenye vifungashio vinavyoonyesha ni bidhaa ya ndani ya nchi.

Akithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wananchi Oktoba 14, walifuatilia jambo hilo na katika upekuzi walikuta mfanyabiashara, Abuu Yahaya, mkazi wa Masanga mkoani Kigoma Ujiji akiwa na mifuko ya sukari 64, yenye thamani ya Sh. 4,824,000 pamoja na madumu ya mafuta ya kula 80 yenye thamani ya Sh. 4,440,000.

"Tumekamata mifuko ya sukari ikiwa na nembo ya Kagera Sugar, wakati ukweli ni kwamba sukari hiyo inadhaniwa kutoka nchini Congo na imefungwa upwa kuonyesha ni sukari kutoka Tanzania," alisema.

Upekuzi huo umefanikisha kubaini mifuko tupu mitano kutoka Zambia, mmoja kutoka Uganda, na kutoka nchini Kagera sugar 18, Kilombero minane na nailoni tupu za kuvisha tano.

Aidha, Manyama alisema mfanyabiashara huyo aliingiza bidhaa kutoka nje ya nchi kimagendo, ili kukwepa ulipaji wa kodi kama utaratibu wa serikali unavyoagiza.

Alieleza bidhaa zinazoingia nchini kimagendo zinaweka hatarini afya ya walaji kwa kuwa mamlaka ya udhibiti ubora haipati nafasi ya kuzithibitisha kama ni salama kwa matumizi ya binadamu.

"Mfano mafuta tuliyokamata yakidhaniwa kutoka nchi ya Kidemokrasia ya Kongo hayana nembo ya ubora kutoka TBS, hiyo ni hatari kwa walaji," alisema.

Rehema Thomas, mkazi wa Kigoma alisema mamlaka ya udhibiti wa bidhaa na vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kuongeza nguvu katika udhibiti kutokana na uwepo wa mipaka mikubwa ya wazi ya nchi kavu na majini.

Pia, alishauri utolewaji wa elimu endelevu kwa wafanyabiashara juu ya madhara ya uingizwaji wa bidhaa kimagendo kwao na kwa serikali pamoja na kuelimisha walaji namna ya kubaini usalama wa bidhaa wanazonunua.



Wanafunzi wakinawa mikono kwenye kifaa kilichotengenezewa na Shirika lisilo la kiserikali la WaterAid, na kutolewa msaada kwa shule mbili za msingi ya Chanzige A na Chanzige B, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani jana, ikiwa ni Siku ya Maadhimisho ya Unawaji Mikono Duniani. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Serikali yaonya matumizi fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa maagizo mazito kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), ikitaka kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, zinawafikia walengwa kwa wakati.

Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, serikali imetenga Sh. bilioni 464 kwa mikopo ya wanafunzi wanaojiunga katika vyuo vikuu na wale wanaoendelea na kozi mbalimbali.

Pia serikali imewataka maofisa mikopo kuhakikisha kuwa wanaratibu vizuri utoaji wa mikopo na ufuatiliaji wa marejesho kwa wanufaika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Leonard Akwilapo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha menejimenti ya HESLB na maofisa wanaosimamia mikopo vyuoni.

Dk. Akwilapo alisema fedha zilizotengwa kwa msimu huu, zimelenga kuwanufaisha wanafunzi 145,000 wanaosoma katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini.

Alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kimekuwa kikiongezeka kila mwaka, ili kutoa fursa kwa vijana wengi wa Kitanzania kupata mikopo ya elimu ya juu, ili watimize ndoto zao.

"Kiasi hichi kimepanda ukilinganisha na kile cha mwaka fedha 2014/15, ambacho ilikuwa Sh. bilioni 347. Hali hii inaonyesha ni namna gani serikali ambavyo imedhamiria kuwezesha vijana wa kitanzania kupata elimu bila kuwa na usumbufu wowote," alisema Dk. Akwilapo.

Pia aliwataka maofisa mikopo vyuoni kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika kuhakikisha wanafanya katika mazingira ya utulivu, bila kuwapo malalamiko yoyote.

"Katika miaka iliyopita pamekuwapo na utulivu katika utoaji wa mikopo, hivyo nawataka maofisa mikopo wote pamoja na vyuo kuhakikisha zoezi hili lifanyika kwa utulivu na wanafunzi wote, wanashughulikiwa nisingependa kusikia malalamiko yoyote," alisema.

Vievile, aliagiza vyuo vikuu nchini vinapopokea fedha hizo, visikae nazo katika akaunti zao bali wawapatie wanafunzi waliokidhi vigezo, bila kuwawekea vikwazo.

Dk. Akwilapo pia alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano, imetumia Sh. trilioni 2.25 kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi mbalimbali wa elimu ya juu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdulrazaq Badru, alisema watahakikisha kuwa kabla ya vyuo vikuu, kufunguliwa mwezi ujao, fedha hizo zitakuwa zimewafikiwa wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo.

Badru alisema utaratibu wa madawati ya maofisa mikopo vyuoni ulianzishwa na serikali rasmi mwaka 2011, ili kusimamia na kuwezesha mikopo na hivi sasa pia yanaratibu urejeshaji wa mikopo.

Alifafanua kuwa katika kikao kazi hicho, kinachoshirikisha maofisa mikopo vyuoni zaidi ya 120, pia mada mbalimbali zitajadiliwa, ikiwamo ulipaji mikopo kidigitali na ufafanuzi wa tozo mbalimbali za mikopo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB, Prof. William Anangisye, aliwataka maofisa mikopo kutumia lugha zenye staha kwa wanafunzi wakati wanapo wahudumia.

Alisema si jambo la busara kusikia kuwa kunakuwepo na malalamiko kwa wanafunzi kuwa maofisa mikopo wanatumia lugha mbaya kwao wakati wa kuwahudumia.

"Wanafunzi wamekuwa wakienda katika vyombo vya habari kulalamika kutokana na nyinyi maofisa mikopo kutoa lugha chafu kwao lazima mfanye kazi kwa kuheshimiana bila kujali nafasi zenu," alisema Prof. Anangisye.

## BoT: Huduma za kibenki kutofungwa uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema huduma za kifedha zitaendelea kutolewa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki, jijini Dar es Salaam, huduma za kibenki zinazotolewa na benki na taasisi za fedha nchini kutolewa kama kawaida.

"Benki Kuu inawataka wananchi kupuuza taarifa potofu zinazosambaa katika mitandao ya kijamii kwamba kuna maelekezo ya kusitisha huduma hizo muhimu katika kipindi cha uchaguzi," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema kama msimamizi wa benki na taasisi za fedha, haijatoa maelekezo yoyote ya kusitisha huduma za kibenki kwa wateja wa taasisi hizo.

"Wananchi wataendelea kupata huduma zote za kibenki kama kawaida wakati wote kabla, wakati na hata baada ya uchaguzi," ilisisitiza taarifa hiyo huku ikitoa onyo kwa wapotoshaji.

# Wizara yatoa tahadhari kwa mvua zinazoendelea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewatahadharisha wananchi kuzingatia kanuni za afya kutokana na mvua zinazonyesha baadhi ya maeneo ikiwamo Mkoa wa Dar es Salaam.

Kutokana na mvua hizo, wizara imesema kuna uwezekano wa kuibua magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara damu na yale yanayoenezwa na mbu kama vile malaria na dengue, iwapo tahadhari hazitachukuliwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, (pichani) alisema uharibifu wa miundombinu umeanza kujitokeza ikiwamo ya kusafirishia na kuhifadhi majisafi na taka jambo, ambalo linahatarisha afya ya jamii.

"Kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kuenea kwa urahisi magonjwa ya kuambukiza na yale ya mlipuko. Kutokana na hali hiyo, wizara inatoa tahadhari kwa wananchi kuchukua hatua za kujikinga na magonjwa haya," alisema.

Aliwataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuendelea kushirikiana na viongozi wengine wa serikali za mitaa, wananchi na wadau mbalimbali, ili kuhakikisha kila eneo haligeuki kuwa chanzo cha magonjwa ya milipuko.

Prof. Makubi alizitaja kanuni wanazotakiwa kufuata wananchi ni pamoja na kuchemsha maji ya kunywa, kuepuka kula chakula kilichopoa, au kuandaliwa katika mazingira yasiyo safi na salama.

Zingine ni kutumia ipasavyo, vyoo na kunawa mikono kwa maji safi na tiririka na sabuni kabla ya kula, baada ya kutoka chooni, baada ya kumnawisha mtoto aliyejisaidia na baada ya kumhudumia mgonjwa.

"Hatua zingine ni kuosha matunda na majisafi kabla ya kula, kuongeza usimamizi wa usafi wa jumla na mikono katika maeneo ya mikusanyiko kama shuleni, vyuoni na sokoni," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka kutotapisha vyoo, kujikinga kuumwa na mbu pamoja na kutumia vyandarua, kusimamia usafi katika mifumo ya majisafi, majitaka na mitaro.



"Nawaomba sana waganga wetu wa wilaya wachukue 'leadership' (uongozi) katika hili na kushirikiana na mamlaka ndani ya eneo lao. Wizara inaendelea kuwakumbusha tiba ni bora kuliko kinga," alisema.


BIASHARA ZOTE MAKINI

HUTANGAZWA HAPA

Nipashe | Nipashe mwendo mdundo

Unafahamu ni kwa nini?

"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII

WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)

PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store | Google Play

KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utolewe mwongozo kuelimisha watoa huduma za fedha

**HIVI** karibuni Benki Kuu ya Tanzania (BoT), iliongeza miezi sita ya maombi ya leseni na usajili kwa watoa huduma za fedha ikiwamo vikundi vya kifedha vya kijamii (VICOBA), SACCOS na vikundi vinginevyo.

Muda uliotolewa tangu Novemba mwaka jana unaisha Oktoba 31, mwaka huu, na kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, yeyote atakayekutwa anatoa huduma hiyo bila leseni atachukuliwa hatua za kisheria.

Kabla ya nyongeza ya muda huo utakaokwisha Aprili 30, 2021, vikundi mbalimbali ambavyo vingi ni vya wanawake vilikuwa katika taharuki kubwa ya namna ya kukimbizana na muda uliosalia ili kujisajili, lakini vilikosa taarifa.

Aidha, vikundi vingi vilijikuta katika wakati mgumu kwa kuwa kila walipokwenda halmashauri au manispaa kwa Maofisa Maendeleo Jamii, waliambiwa wajisajili na kulipa ada ya Sh. 50,000 wakati wanasubiri mwongozo wa BoT na namna watakavyopata leseni ya kuendesha vikundi vyao. Vikundi hivi ni vya watu walioungana kwa lengo la kupambana na umaskini, yaani kupitia katiba zao wameweka makubaliano ya namna watakavyoweka mtaji au hisa anzia. Pia, vikundi hivyo vina taratibu tofauti ikiwamo kuvunja vibubu kila baada ya miezi 12 kwa kuchukua fedha zote na kuanza mzunguko upya na wengine huchukua hisa, lakini fedha ya mtaji hubaki kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa mikopo.

Vikundi hivyo hutoa mikopo kwa wanachama kulingana na viwango walivyokubaliana, riba na muda wa kurejesha na fedha zote haziruhusiwi kuvuka mwaka, huku wengine wakienda mbali zaidi kutoa mikopo ya maendeleo kuwawezesha wanachama wasio na vyombo vya usafiri kuvimiliki, au wasio na nyumba kuanza ujenzi. Pia, hutoa mikopo kwa ajili ya kuanzisha biashara, na lengo kubwa ni kuwawezesha kujikwamua kwa kutumia fedha za wanachama ambazo huzunguka kutoka kwa mmoja hadi mwingine.

Hakuna ubishi vikundi hivi ni mkombozi kwa wanawake wengi kwa kuwa ndiko walikopata mtaji wa kuanzisha biashara, kumiliki vyombo vya usafiri, nyumba, kusomesha watoto katika shule nzuri, matibabu na kulipa kodi za nyumba.

Wanawake kupitia uwekezaji huo wamejipatia mitaji na kuondokana na adha ya kukopa benki ambako riba si rafiki na hakuna cha kuweka rehani ili kupata fedha hizo.

Katika jitihada hizo zilijitokeza changamoto kama za baadhi ya wanachama kukimbia na fedha za wenzao kiasi cha kupelekana polisi, na ndipo serikali ikaja na utaratibu ikiwamo kuwa na sheria ya kuhudumia vikundi hivi.

Lengo ni zuri, lakini bado wanachama wa vikundi hivi wamejikuta katika taharuki kiasi cha wengine kufikiria kuvunja kabisa, kwa kuwa hadi sasa haiko wazi kiasi cha kodi ambacho kitatozwa katika fedha za wanachama walizokusanya na kukopeshana.

Na bahati mbaya baadhi ya Maofisa Maendeleo ya Jamii wameshindwa kuelimisha wanavikundi, zaidi ya kuwataka kulipa fedha na kuweka viambatisho, huku kukiwa na maswali baada ya hapo nini kinafuata? Je, ndiyo kikundi kimesajiliwa? Watapata wapi leseni? Kabla ya mwongozo huo wapo waliokwenda mbali zaidi kwa kuamua kugawana fedha zao, ili kubaki salama kabla ya kukatwa au vinginevyo, lakini yote hiyo ni kukosekana kwa taarifa ngazi za halmashauri wanakokwenda kujisajili.


Tunasema muda ulioongezwa utumike vizuri kwa vikundi kufuata utaratibu wa kujisajili, lakini ni vyema BoT ikaweka wazi mwongozo na kodi zitakazotozwa kwenye vikundi hivi. Taarifa zilizopo halmashauri bado hazijitoshelezi na vikundi vingi ambavyo vinatoa huduma za kijamii vinakwenda ngazi hiyo kupata uelewa wa kina kwa ajili ya kuwafikishia wanachama wao.

Ikiwa wanachama wataona na kusoma mwongozo husika maana yake hakutakuwa na taharuki wala maswali mengi yasiyo na majibu hasa katika usalama wa fedha zao ambazo zinahifadhiwa katika benki mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kunahitajika elimu zaidi ya matumizi 'zebra' barabarani

Na Christina Mwakangale

**KIVUKO** cha watembea kwa miguu (zebra crossing), maarufu pundamilia, ni alama maalumu inayochorwa kwa rangi nyeupe barabarani kwa watu kuvuka.

Katika barabara zote zilizo na lami na kuwa na alama hiyo, wanalindwa na Sheria ya Usalama Barabarani.

Pamoja na hilo, kuna baadhi ya wenye vyombo vya moto kutoheshimu vivuko hivi na kusababisha ajali.

Madereva wa magari na bodaboda, ingawa kwa kiasi kikubwa nawaingiza katika kundi kubwa la wanaoendesha vizuri, wapo wachache kati yao wasioheshimu nidhamu na sheria za barabarani na katika nafasi ya pekee, penye alama za pundamilia. Ukiwa mtumiaji wa barabara unapoenda kwenye shughuli zako za kila siku, hasa maeneo ya mijini utashuhudia hili, licha ya kuwapo nadharia ya madereva wengi wa magari hivi sasa wameelimika na kuheshimu maeneo haya.

Shida kubwa huwa naishuhudia kwa waendeshaji bodaboda, ambao ni wazito penye alama hizo za kiusalama. Baadhi hawasimami, ilhali wamekuta magari yamesimama mahali hapo, kuruhusu watu kuvuka.

Ndugu hawa wa bodaboda, wana miongozo pori ya kwao hata usishangae, taa za kuongoza magari ikiwaka nyekundu wao wanaona maana yake 'vuka' na kijani au njano anaweza akasimama.

Licha ya bodaboda kuajiri vijana wapatao milioni 1.5 nchini, huku usafiri huo ukitegemewa na watu wengi husussan makazi ya mijini ili kurahisisha safari, elimu ya kuziheshimu zebra zinapaswa ziendelee kutolewa.

Ajira hii kubwa kwa vijana, wanapaswa waelimishwe kuhusu matumizi na kanuni bora za barabarani, ili isiwe na madhara kwa jamii, kwa kuwa ajali zina madhara makubwa ya kiafya katika jamii. Hapo kuna hesabu ya ulemavu, vifo na hata kuongeza idadi ya wategemezi, katika hali ambayo huenda ingezuilika.

Ajira hii isiyo rasmi, inakadiriwa iwapo bodaboda mmoja akifanyakazi ya Sh. 5,000 kwa siku ikizidishwa mara idadi yao milioni moja na nusu, kuna makusanyo ya fedha wastani wa shilingi bilioni 7.5 kila siku.

Ni hesabu kubwa ya mapato na kwa maana hiyo, ni shughuli serikali inapaswa kuendelea kudumisha, kuptoa maboresho ya usalama barabarani.

Utamaduni wa zebra haukuanza miaka ya karibuni, kwani historia inaonyesha takribani miongo sita tangu kuanzishwa huko nchini Uingereza.

Takwimu za taasisi hiyo zinaonyesha kati ya majeruhi 2,223 waliolazwa Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Muhimbili (MOI), mwaka 2016, zaidi ya majeruhi 1,100 wa barabarani waliumizwa kupitia bodaboda.

Jiji la Dar es Salaam, lina wakazi takribani milioni tano na kuna matumizi ya usafiri wa aina tofauti, ikilinganishwa na maeneo mengine nchini.

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, linasema nusu ya ajali zote zilizotokea nchini, asilimia 53 zilitokea jijini Dar es Salaam kati ya Januari na Machi mwaka 2019.

Linasema kati ya ajali hizo 776 zilizotokea nchini kwa kipindi hicho, ajali 416 zilitokea Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2016 zinasema kuwa watu milioni 1.4 walipoteza maisha katika ajali za magari duniani. Hapo inajenga ujumbe wa kiusalama kwamba, wakati watembea kwa miguu wakizingatia kuvuka katika alama ya zebra, barabarani, ni wajibu wa madereva kuheshimu kila waonapo dalili ya anayetaka kuvuka, ili wampishe avuke.

Wataalamu wa masuala ya barabarani, wanaeleza kuwa kila aliye jirani na zebra au anayetarajia kuvuka aheshimiwe kwani amefuata sheria.

Hatari za ajali barabarani katika nchi zinazoendelea, ziko kiwango cha juu kwa mara tatu zaidi, huku WHO ikisema kwamba kuna vifo 27 kwa kila watu 1000.

Vifo vya barabarani katika nchi za Afrika ni mara tatu zaidi ya ajali zinazotokea barani Ulaya, ambako kuna ajali chache zaidi.

Ripoti ya WHO iliyotolewa mwaka 2018, inabainisha kuwa Sheria za Tanzania kwa upande wa usalama barabarani zina upungufu katika kudhibiti usalama barabarani, katika baadhi ya maeneo.

Kuna shida kuhusiana na tabia ya kuruhusu ulevi mkubwa kwa madereva, jambo ambalo ni hatarishi.

Tanzania imeweka ukomo wa kilevi kuwa ni wastani kitaalamu gramu 0.8 kwa kila desimali lita (0.08g/dl), lakini WHO inaeleza dereva mwenye kiwango hicho cha ulevi anakuwa hatarini kupata ajali mara nne zaidi ya yule ambaye hajatumia pombe kabisa. WHO pia inashauri ni vizuri ukomo wa ulevi ukawa ni wastani wanaoutaka gramu 0.05 kwa kila desimali lita (0.05g/dl) kwa madereva wazoefu na wasio na uzoefu ni gramu 0.02g/dl kwa madereva wapya.

Kutokana na ajali hizo, ni wakati wa madereva na watembeaji kwa miguu, kuheshimu sheria za usalama barabarani kupunguza vifo vitokanavyo na ajali.

HABARI KITAIFA

# Ardhi yaanzisha mkakati wa kufuatilia ucheleweshaji hati

**Na Munir Shemweta,**
BABATI

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Manyara imeanza mkakati maalum wa kwenda ofisi za ardhi katika halmashauri kuzifuatilia hati, ambazo haziwasilishwi kwenye ofisi hiyo kwa wakati, ili kujua changamoto na kuzitafutia ufumbuzi.

Mkakati huo unatokana na ofisi hiyo kuzishambulia kwa nguvu hati zilizopelekwa katika ofisi hiyo zikiwamo zilizokuwa na marekebisho na kuzimaliza zikitokea iliyokuwa Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kaskazini (Moshi) iliyojumuisha mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Hayo yalibainishwa jana na Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Manyara, Leonard Msafiri, wakati akielezea utendaji kazi wa ofisi yake tangu na kuzinduliwa rasmi Julai, mwaka huu na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi

"Sasa tumeamua kuja na mkakati maalum wa kwenda katika wilaya kuzitafuta hati zilizoko kule kwa nini haziji na kwa nini haziendi kwa kasi kubwa," alisema Msafiri.

Kwa mujibu wa Msafiri, tayari ofisi yake imeanza kuzifanyia kazi baadhi ya changamoto za sekta ya ardhi katika halmashauri za mkoa huo na kutolea mfano Halmashauri ya Wilaya ya Babati katika suala la uandaaji wa 'deed plan'.

"Katika kutekeleza mkakati wetu, tumewapeleka wataalamu wetu wawili wa upimaji na ramani kuangalia ramani zinazotakiwa kuandaliwa katika Halmashauri ya Babati na tutaendelea halmashauri nyingine," alisema.

Wataalamu watakapofika ofisi za ardhi za halmashauri husika, alisema, wataitisha majalada ya ardhi ya watu walioomba kumilikishwa na kuyafanyia kazi na kuangalia changamoto za msingi kama zipo na yatakapokamilika wataondoka nayo.

Msafiri alisema ofisi ya ardhi mkoa wa Manyara tangu kuanza kazi Machi, mwaka huu, imeandaa na kugawa hati kwa wamiliki wa ardhi takriban 350 na kubainisha kuwa lengo la ofisi yake ni kuhakikisha hati zote zinazowasilishwa zinakamilishwa ndani ya wiki moja na kupelekwa kwa wahusika.

Kuhusu urasimishaji katika mkoa wake, Msafiri alisema kazi hiyo inaendelea vizuri huku akibainisha kuwa changamoto kubwa iliyojitokeza ni kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto iliyokuwa ikichukua asilimia 15 ya fedha inayotolewa na wananchi kwa mkandarasi na kufifisha kasi ya kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Msafiri, ofisi yake ilitembelea uwanjani na kuzungumza na uongozi, mkandarasi na wataalam wa ardhi kuhusiana na suala hilo na kuagiza kusitishwa makato hayo na fedha kidogo zinazotolewa na wananchi ziingie kwenye mradi, ili ukamilike na hati zikitolewa zitaandaliwa ankara zitakazoingizwa madeni na asilimia itoke wakati kazi imekamilika.

Kuhusu migogoro ya ardhi, alisema tangu kuanzishwa ofisi ya ardhi mkoa wa Manyara wamehakiki mashamba yote na kuanza kuyafanyia kazi yenye migogoro. Alitolea mfano wa shamba lililoko Mawemairo, Magugu lenye ukubwa wa ekari 111, ambalo wananchi walilalamika kuwa wamenyang'anywa.

Msafiri alisema baada ya kulikagua eneo hilo kwa ushirikiano na walalamikaji, walibaini kuwa shamba hilo halikuvamiwa bali uelewa mdogo wa walalamikaji ndiyo uliosababisha mgogoro huo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Arch. Elius Mwakalinga (kulia), akitoa cheti kwa Mkurugenzi Mtendaji Lock $ Door Systems Joshua Munguti, kwa kutambua udhamini wa kampuni hiyo, katika mkutano wa mwaka wa bodi ya usajili wa wabunifu wa majengo na wakadiriaji majenzi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Maalim Seif azuiwa kampeni kwa siku 5

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif, amezuiwa kufanya kampeni kwa muda wa siku tano kuanzia leo hadi Oktoba 20.

Adhabu hiyo imekuja baada ya Kamati ya Maadili ya Uchaguzi kutoa uamuzi huo kutokana na mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Demokrasia Makini, Ameri Hassan Ameri, kutoa malalamiko lake dhidi ya Maalim Seif.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Kamati ya Maadili ya Tume ya Uchaguzi, Khamis Issa Khamis, alisema mlalamikaji alipeleka lalamiko lake dhidi ya Seif kuwahamasisha wafuasi wake kwenda kupiga kura Oktoba 27, siku ya uchaguzi wa kura za mapema ambazo hupiga watu maalum.

"Katika mkutano wake wa Oktoba 13 huko Jadida Pemba, Maalim Seif alitoa kauli ya kuhamasisha wanachama wake kwenda katika vituo vya kupigia kura siku ya Oktoba 27, kinyume na kifungu 18(1) (2) cha Sheria ya Uchaguzi ambacho kimewataka watu maalum ambao ni wasimamizi wa uchaguzi na vyombo vya ulinzi na usalama vinavyosimamia uchaguzi," alisema.

Khamis ambaye ni Mwanasheria wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, alisema kamati ya maadili baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili kuhusu malalamiko hayo, imekubaliana kwa pamoja kuwa mlalamikiwa katika shauri hilo amefanya kosa la kimaadili kwa kutoa kauli ya kuwashawishi wafuasi wake wote kwenda katika vituo vya kupigia kura Oktoba 27, kitendo ambacho ni uvunjifu wa maadili.

Alisema wagombea wote 17 wa urais wa Zanzibar walisaini kuwa wataziheshimu na kuzifuata taratibu za kampeni zao.

Kadhalika, alisema Kamati ya Maadili imeamua kutoa adhabu hiyo chini ya kifungu cha 23 (d) cha kanuni za maadili ya uchaguzi ya mwaka 2020.

Vile vile, kwa uamuzi huo mikutano ya mgombea wa urais wa ACT-Wazalendo kwa tarehe hizo imefutwa katika ratiba ya kitaifa ya kampeni. Alisema mgombea huyo ana haki ya kukata rufani ikiwa hakuridhika na uamuzi wa kamati.

# Wataalamu ujenzi wasiosajiliwa kukiona

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema kuanzia Januari, mwakani, itaanza kuchukua hatua dhidi ya kampuni za wabunifu majengo na wakadiriaji ujenzi, ambao hawajasajiliwa.

Akizungumza katika mkutano wa kwanza wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alisema kampuni zinazofanya kazi hizo zinapaswa kujisajili kabla ya kukumbwa na mkono wa sheria.

Alisema lengo ni kuhakikisha kwamba kila anayefanya shughuli hizo awe ni mtaalamu na si kuwaachia wasio na taaluma kufanya shughuli hizo.

"Hii ni taaluma muhimu na nyeti kwa uchumi wa nchi yetu. Tuko katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na juhudi hii haiwezi kufikiwa katika malengo yake kama hakuna wataalamu wa uhakika katika sekta hii, ndiyo maana tunataka tuhakikishe wote wanasajiliwa na tunawatambua," alisema Mwakalinga.

"Na tunataka shughuli zote sifanywe na wataalamu na si kuruhusu watu wasio sahihi kuvamia sekta hii na kuharibu. Usajili huu utarahisisha kuwatambua wavamizi na kuwachukulia hatua kali za kisheria. Lengo ni kuongeza udhibiti wa shughuli za wataalamu wasiosajiliwa na kufanya kazi, bila kuwa na leseni."

Mwakalinga pia alisema kwa sasa serikali inaandaa mfumo maalum wa ufuatiliaji wa uendeshaji wa vivuko nchi nzima kwa kufunga vifaa maalum (GPS) ambavyo vitasaidia kurekodi uendeshaji wake.

Alisema pamoja na mambo mengine mfumo huo unalenga kudhibiti uharibifu wa miundombinu na kusaidia kupunguza ajali zisizo za lazima.

"Hatua hii ya kufunga GPS iko kwenye mchakato na tunatarajia kwamba mpaka Januari mwakani tutakuwa tumekamilisha. Mfumo huu utatusaidia pia kufahamu pale kivuko kinapozidisha mzigo au kufanya shughuli zake kinyume na taratibu, hata tukiwa ofisini tutakuwa tunaona," alisema Mwakalinga.

Msajili wa Bodi hiyo, Edwin Nnunduma, alisema mpango wa kusajili kampuni na wataalamu katika sekta hiyo utasaidia kupunguza malalamiko mengi, ambayo wamekuwa wakipokea kutoka kwa baadhi ya wavamizi wa taaluma hiyo pale wanapoharibu kazi.

Nnunduma alisema hadi Septemba, mwaka huu, bodi ilikuwa imesajili wataalamu 1,126 na kampuni za kitaalamu 381.

"Wakati bodi inaanza wataalamu waliosajiliwa walikuwa 188 na kampuni za kitaalamu 53. Ongezeko hili ni kubwa, lakini ukilinganisha na uhitaji wa huduma za wataalamu nchini, idadi hii bado ni ndogo," alisema Nnunduma.

# Mufti Zubeir ataka amani ilindwe uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

MUFTI wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, amewataka Watanzania wa dini zote kuitunza amani waliyopewa na Mungu kuelekea katika uchaguzi mkuu unaopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mufti Zubeir alisema huo ni ujumbe wake kwa Watanzania wa dini zote.

Alisema amani inatakiwa kuhifadhiwa kwa sababu ikivunjika siyo rahisi kuirejesha.

"Tusikubali kupitishwa katika viashiria vya aina yoyote vinavyoweza kuvunja amani, viwe vya maneno, vitendo, au ishara, tusikubali kuvipokea na kushikamana navyo," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema wananchi wasikubali kuingizwa katika maangamizi ya kuvunja amani na kuiacha nchi isiyokalika. "Kwa kufanya hivyo, maana yake mtakuwa mmevunja amri ya Mungu anayosema msiingize mikono yenu kwenye maangamivu," alionya.

Alisema nchi ambazo zimevunja amani, zimekuwa na matatizo makubwa kwa kusababisha watu wengi kuangamia wakiwamo wasio na hatia, hususan wanawake na watoto.

Alisema mambo ambayo yanaweza kuitunza amani ni kuimarisha uzalendo kwa kuipenda nchi na kuzuia kila aina ya vurugu itakayoondoa sifa hizo.

"Kukosa uzalendo katika dini ni kukosa imani na kukosa imani ni kuwa nje ya dini na malipo yake ni Mungu kukuadhibu na kukutayarishia makazi mabaya," alisema.

"Katika mambo yanayoweza kujenga mshikamano ni kujenga umoja baina yetu kama Watanzania na kutengeneza mshikamano na kujenga mapenzi, haya yatajenga namna ya kulinda amani. "Haya yanakusanywa na tabia njema, tabia kwa kawaida ni jambo linalotengenezeka, kama ana tabia mbaya akawa na tabia nzuri."



Moja ya eneo la Mtaa wa King'azi B, Kata ya Kwembe, likiwa limeharibiwa na mvua zilizonyesha jijini Dar es Salaam jana, licha ya jitihada za kuweka viroba vya mchanga na matairi ili kuzuia mmomonyoko. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vyuo vikuu vyamwenzi Mwalimu Nyerere

**Na Vincent Mpepo,** CKHT

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania Kituo (CKHT) Mkoa wa Mbeya, kitaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kitaaluma na zisizo za kitaaluma mkoani humo katika kuhakikisha kwa pamoja wanachochea maendeleo.

Mhadhiri na Mkurugenzi wa Kituo cha Mbeya cha chuo hicho, Maulana Ali, alitoa kauli hiyo jana wakati wa Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere lililofanyika chuoni huko.

Alisema madhumuni ya kongamano hilo ni kuwakutanisha wanataaluma na wasio wanataaluma, ili kujadili masuala mbalimbali kuhusu Mwalimu Nyerere ambaye ni Baba wa Taifa na mchango wake kwa taifa.

"Kwa mwaka huu, kongamano limejikita katika kuangalia mchango wa Mwalimu Julius Nyerere katika lugha ya Kiswahili na falsafa zake kuhusu uchaguzi," alisema Maulana.

Akiwasilisha mada kuhusu 'Mwalimu Julius Nyerere Kama Mwanahistilahi wa Kiswahili', Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji-Mbeya, Profesa Hermas Mwansoko, alisema Mwalimu Nyerere alifanya kazi nyingi za kitaaluma ambazo zimechangia kukuza lugha ya Kiswahili.

Alisema licha ya kuwa na talanta ya uongozi, Mwalimu Julius Nyerere alifanya kazi mbalimbali za uandishi wa vitabu na matini mbalimbali, tafsiri ya vitabu na kushiriki kwa namna moja au nyingine katika uundaji wa msamiati na istilahi mbalimbali.

Mhadhiri wa CKHT, Matilda Ngonje, alisema Mwalimu Nyerere bado anatazamwa na wasomi na wanasiasa wengi wa ndani na nje ya nchi katika kutafakari masuala mbalimbali ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Alisema Mwalimu Nyerere aliamini utekelezaji wa demokrasia katika nchi za kiafrika unatokana na muktadha, mazingira na nyakati halisi zinazosawili nchi husika.

"Mwalimu Julius Nyerere aliamini kuwa demokrasia ya kitanzania inasawili mazingira ya kitanzania," alisema Matilda.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Kampasi ya Mbeya, Salvatory Mhando, alisema falsafa ya Mwalimu Nyerere bado inafaa kwa kuwa inaangalia uhalisia wa ufanyikaji wa siasa una uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni wa nchi husika.

Alisema hatuwezi kufananisha siasa za nchi za kiafrika kama Tanzania na Ugiriki au Marekani kwa kuwa lazima tukubali kuna utofauti kutokana na mazingira ya kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi.

## RUWASA yakumbushwa kuwajengea uwezo wateja

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), umetakiwa kuhakikisha Jumuiya za Watumiaji Maji (CBWSOs) zinakuwa na uwezo wa kupanga, kukusanya na kusimamia maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji, ili kuwa na miradi endelevu.

Maelekezo hayo yalitolewa mkoani Mwanza na Mwenyekiti wa Bodi ya RUWASA, Profesa Idrissa Mshoro, wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha maofisa wa RUWASA kutoka mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Pwani na Simiyu.

Profesa Mshoro alisisitiza kwamba, ili miradi inayotekelezwa na RUWASA iwe endelevu, ni lazima Jumuiya za Watumiaji Maji (CBWSOs), wakajengewa uwezo kuanzia hatua za awali.

"Menejimenti mnatakiwa kuimarisha uwezo wa jumuiya kwa mipango madhubuti ya kujenga uwezo, kudhibiti na kusimamia taasisi na huduma, CBWSOs ziwe na uwezo wa kupanga, kukusanya na kusimamia maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji yatakayowezesha uendeshaji na matengenezo ya mradi," alisisitiza Profesa Mshoro.

Aliwaelekeza watendaji wa RUWASA kuimarisha uhusiano na ushirikiano na taasisi zingine zikiwamo ofisi za Mabonde, Mamlaka za Maji, ofisi za Serikali za Mitaa, Halmashauri na Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mikoa, ili kufikia malengo na mipango walionayo.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa halmashauri kutopata taarifa za RUWASA kama inavyopasa na kuelekeza watendaji kuwasilisha ripoti zao, kwenye ofisi za halmashauri, mikoa na wilaya kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Profesa Mshoro aliitaka Menejimenti ya RUWASA kuonyesha njia kwa kudumisha dhana ya ushirikiano katika ngazi ya mipango, bajeti na mawasiliano na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji.

"Undugu huo wa uasili na usambazaji wa rasilimali maji unafanya kusiwe na mjadala katika umuhimu na ulazima wa kushirikiana kwa taasisi hizi; tutumie fursa ya mtazamo, msimamo na msisitizo wa Wizara ya Maji katika ufanyaji kazi kama wizara moja, huduma moja, mlengwa mmoja," alielekeza Profesa Mshoro.

# Kortini tuhuma za uhujumu uchumi

Na Hellen Mwango

WATU wawili; Mhandisi Baraka Mtunga (43) na mfanyabiashara Rajabu Katunda (42), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) hasara ya Sh. milioni 267.6.

Mtunga na Katunda, wote wakazi wa Mikocheni wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, walifikishwa juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Kassian Matembele.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Jacqueline Nyantori na Yusuph Abood, ulidai washtakiwa walitenda kosa hilo katika tarehe tofauti kati ya Desemba 13, 2019 na Septemba 28 mwaka huu maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan katika Kijiji cha Kajanjoo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani na maeneo ya Jiji la Dar es Salaam.

Simon alidai washtakiwa kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Alidai kuwa kati ya Desemba 13, 2019 na Septemba 28 mwaka huu, maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan katika Kijiji cha Kajanjoo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, washtakiwa hao walisimika na kutumia vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki bila kuwa na leseni ya TCRA.

Pia, alidai washtakiwa hao walitumia vifaa vya kielektroniki kusambaza mtandao wa intaneti bila kuwa na leseni.

Nyantori alidai katika tarehe na maeneo hayo ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan katika Kijiji cha Kajanjoo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, washtakiwa wakiwa na nia ya kukwepa kulipa malipo halali ya mtandao, walisambaza huduma ya mtandao (WiFi) isivyo halali.

Inadaiwa washitakiwa hao kwa pamoja waliisababishia TCRA hasara ya Sh. 267,656,794.30.

Ilidaiwa washtakiwa hao kwa pamoja walijihusisha na miamala hiyo ya kifedha huku wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya kutumia vifaa vya mawasiliano kwa ulaghai na uhalifu wa kupangwa.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo uliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Matembele aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 27, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa walirudishwa rumande kwa sababu mashtaka yanayowakabili hayana dhamana kisheria.




Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Mkoa wa Morogoro, Mwadhini Myanza (wa pili kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Peak Performance, Phillemon Kisamo, jijini Dar es Salaam, baada ya kusaini makubaliano ya kuwapo kwa programu ya maandalizi kwa wafanyakazi na wanachama wa chemba hiyo, kabla ya kustaafu. Wengine ni Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Upendo Kimbe (kushoto) na Meneja wa Ofisi ya Chemba hiyo, Moumin Mwatawala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto yatima wakumbukwa

**Na Stephano Mango,** SONGEA

WATANZANIA wametakiwa kuwa na moyo wa upendo na huruma kwa watoto yatima na wanaishi katika mazingira magumu kwa kuwasaidia mahitaji muhimu ya kibinadamu ili kufarijika na kuishi kwa amani, furaha kama walivyo watoto wenye wazazi.

Wito huo ulitolewa juzi kwenye kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu Chipole wakati wa kukabidhi maziwa ya unga maboksi 50 yenye maziwa makopo 600 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 12 .

Katibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Saint Theresa Orphans Foundation (STOF), Moses Nyirenda,

alisema kuwa kusaidia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu ni miongoni mwa ishara njema ya kuwaonyesha watoto hao upendo, wema, utu na huruma katika ustawi wao na jamii ijayo. Alisema kuwa watoto ambao wanaishi katika kituo hicho wanatoka katika maeneo mbalimbali katika mkoa wa Ruvuma, ambao familia zao hazina kipato, huku wengine wakiokotwa baada ya kutelekezwa na wazazi wao baada ya kuzaliwa, hivyo kuwasaidia mahitaji yao ni kuonyesha kuwajali na kuwathamini katika maisha yao.

# Watoto wa kike wapewa mbinu kukabili vishawishi

Christina Mwakangale

WATOTO wa kike wameshauriwa kujithamini na kutambua mabadiliko ukuaji ikiwamo kukabiliana na vishawishi vinavyosababisha mimba shuleni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), Tabitha Bugali, aliyasema hao wakati wa madhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike inayoadhimishwa Oktoba 11, kila mwaka.

Alisema mimba katika umri mdogo zinafifisha ndoto za wasichana hivyo wapatiwe elimu kutambua haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Sauti ya Mama Africa Foundation ni Asasi isiyo ya Kiserikali, inajihusisha na wanawake na vijana hasa mtoto wa kike ambaye kutokana na mifumo dume, kandamizi inamnyima haki.

"Kwa kulitambua hilo, tunaendesha kutoa elimu kwa vijana walio ndani na nje ya shule kuona mtoto wa kike anajikomboa kielimu ili kufikia ndoto zake," alisema Bugali.

Pia alisema asasi hiyo inatoa elimu ya ujasiriamali kwa wasichana walee pekee 'single mothers' na kuwaunganisha na taasisi zinazoshughulisha kuanzisha vikundi vya kuinuana kiuchumi.

"Wanapokuwa wamejiunga kwenye vikundi wataweza kukopeshwa na halmashauri, kutokana na elimu hii katika shule nyingi tulizopita ufaulu umeongezeka, mimba zimepungua," alieleza Bugaii.

Alisema kati ya shule zilizopewa elimu hiyo jijini Mbeya ni pamoja na Shule ya Sekondari Sinde na za Msingi Mabatini, Simike na Mbata.

# Wapewa ndoo, sabuni kujikinga magonjwa mlipuko

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KINAMAMA wasiojiweza wanaoishi Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga, wamepewa msaada wa ndoo za majitiririka na sabuni, kwa ajili ya kuzingatia usafi wa nyumbani na kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Kipindi cha janga la maambukizi ya virusi vya corona, wananchi walikuwa wakizingatia usafi wa hali ya juu kwa kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na majitiririka, na hakukuwa na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na kuhara.

Msaada huo umetolewa jana na Shirika la Young Women Christian Association (YWCA), kwa ufadhili wa Shirika la Firelight, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wao wa kuimarisha afya ndani ya jamii, pamoja na lishe na usafi wa kinamama wenye watoto walio chini ya umri wa miaka sita.

Katibu wa Shirika la YWCA, Marysiana Makundi, akizungumza wakati wa kutoa msaada huo, alisema ili kuendelea kukabiliana na magonjwa ya mlipuko hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye msimu wa mvua, ni vyema wananchi wakaendelea kuzingatia usafi.

"Tumetoa msaada wa ndoo 30 za maji tiririka pamoja na madumu ya sabuni kwa kinamama ambao hawajiwezi hapa Ibadakuli, lengo likiwa ni kuendelea kuihamasisha jamii kuchukua tahadhari ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko licha ya janga la corona kuisha," alisema Makundi.

Naye Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli, Sara Wankuru, aliwataka kinamama hao ambao wamepewa msaada huo, wakazitumie ndoo hizo za majitiririka kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Rehema Nkinda, akishukuru kwa niaba ya kinamama wengine, aliahidi kwenda kuzitumia vizuri ili wajikinge na magonjwa ya mlipuko na familia zao kubaki salama.

# Wanahabari kumwenzi Nyerere kimaandishi

**Na Robinson Wangaso,**
BUTIAMA

WAANDISHI wa habari mkoa wa Mwanza na Mara wamesema watashirikiana na familia ya Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Nyerere, kumwenzi kwa kuweka mambo muhimu na aliyoyaishi na kuyapigania katika kumbukumbu za maandishi ili jamii hasa vijana waliozaliwa baada ya kifo chake waweze kuyafahamu.

Walitoa ahadi hiyo Mwitongo nyumbani kwa hayati Baba wa Taifa, wakati wa kumbukizi ya miaka 21 baada ya waandishi wa mikoa ya Mwanza na Mara kufanya ziara na kukutana na mtoto wake, Madaraka Nyerere.

Wenyeviti wa klabu za waandishi wa habari mikoa hiyo, Edwin Soko (Mwanza) na Robinson Wangaso (Mara), walisema wataanzisha utaratibu wa kuitembelea familia hiyo ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wanafamilia ili kuweka kumbukumbu muhimu za Mwalimu ambazo hazijulikani vizuri hasa kwa kizazi kipya.

Wangaso alisema moja ya jambo muhimu ni kuanzisha 'Kifimbo day' ambayo wanaume watahimizwa siku hiyo kutembea na fimbo ya mfano aliyokuwa nayo Nyerere ikiwa ni hatua ya kumwenzi na kukumbuka aliyoyapigania.

Soko, alisema wanahabari wana fursa ya kuyapa umuhimu wa kuyatangaza na kuyaingiza katika kumbukumbu kama urithi wa vizazi ambavyo havikumuona Mwalimu Nyerere wakati wa uhai wake.

Alisema waandishi wa habari wataweka utaratibu mzuri wa kukutana na familia ya Baba wa Taifa ili kuandaa na kutunza katika maandishi kumbukumbu sahihi zinazomhusu.

Kwa upande wa familia ya Baba wa Taifa ikiwakilishwa na mtoto wake, Madaraka, alipokea wazo hilo na kuahidi ushirikiano kwa wanahabari na wadau wengine katika kulitekeleza jambo hilo la kihistoria.

Katika hatua nyingine, Madaraka aliwaasa wanasiasa kumwenzi Baba wa Taifa kwa kutobaguana kwa misingi ya itikadi za vyama hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28.

Alisema baba wa taifa hakuwa na ubaguzi na alishirikiana na watu wa itikadi zote hata wakati wa uhai wake alipokea viongozi na wagombea wa vyama vyote na kufanya nao majadiliano hivyo wanasiasa wanapaswa kuiga mfano huo katika mambo ya maendeleo na kuacha maslahi yao binafsi na vyama vyao ili kudumisha udugu na mshikamano.

Alisema Mwalimu aliamini katika majadiliano kuwa ndiyo njia ya kufikia uamuzi sahihi hivyo alithamini mawazo ya kila mtu.




Naibu Mkurugenzi wa Halotel, Nguyen Van Trung, akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya kampuni hiyo kwa maadhimisho ya miaka mitano ya utoaji huduma za mawasiliano nchini. Pembeni ni Ofisa Uhusiano, Stella Pius. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halotel yasherehekea miaka 5 ya huduma

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ya robo ya pili ya mwaka imeonyesha Kampuni ya Viettel (Halotel), kufikia idadi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zaidi ya milioni sita hadi kufikia Juni, mwaka huu.

Halotel, jana imesherehekea miaka mitano ya utoaji huduma za mawasiliano nchini na kufikia malengo ya juu ikiwamo kuongeza watumiaji wa mtandao huo.

Taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo ilisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mkubwa wa Serikali ya Tanzania kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, pia Watanzania kwa ujumla ambao ni wateja wao, wafanyakazi wa Halotel pamoja na ubunifu wa kampuni hiyo kutengeneza huduma zinazokidhi na mahitaji ya watumiaji.

Akiongea na waandishi wa habari, Naibu Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Nguyen Van Trung, alisema; "Halotel imekuwa ikitoa huduma ya intaneti kwa shule za msingi na sekondari za serikali, imeunganisha mawasiliano kwa ofisi za serikali kuanzia ofisi za wilaya, vituo vya polisi na ofisi za posta kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufasaha."

"Halotel ni mtandao wa kwanza kupeleka mawasiliano kwenye vijiji 4,000 ambavyo havikuwa na mawasiliano tangu Tanzania ilipopata uhuru na kusisimua maendeleo ya wakazi wa vijiji hivyo," alisema Trung.

Alisema kama wawekezaji wengine Halotel imekuwa mstari wa mbele kwa kusaidia jamii kufikia maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya kiafya, elimu, mawasiliano, michezo, kilimo na watu wenye uhitaji maalumu kwenye jamii.


"Pia tunafurahia kuona Watanzania hivi sasa wameshika nafasi kubwa za uongozi (menejimenti) makao makuu na katika matawi yetu ya nchini. Haya ni mafanikio makubwa kuona kampuni inaendeshwa na kusimamiwa na Watanzania," alisema Trung.

Katika kusherehekea miaka mitano, Halotel imezindua ofa maalum zitakazo wawezesha wateja wake kuwasiliana kwa punguzo kubwa. Hii ni mara ya kwanza kwa Halotel kutoa ofa kubwa kwa wateja wake na ofa hizo zinajulikana kama, "Dabo bando" na kuongea bure Halotel kwenda Halotel pia kwa wateja watakuwa wakipata zawadi mbalimbali ikiwamo vocha watakapo tembelea maduka ya nchi nzima ndani ya mwezi huu.

Pia, Trung alizindua ofa maalum ya Halopesa ya "kurudishiwa asilimia 50 ya makato ya kutuma pesa" kwa mtandao wa Halotel na mitandao mingine kwa muda wa siku tatu kuanzia Oktoba 15 hadi 17. Wakala na washirika wa Halopesa watapata zawadi na hati za shukurani.

## Kufanya kazi kwa pamoja kubadilisha kilimo vijijini Tanzania

Ukurasa 14



## Kutokomeza utapiamlo iko ndani ya uwezo wetu

Ukurasa 13





Ukurasa 12

## Ufugaji sungura umeboresha upatikanaji wa chakula bora katika kijiji cha Mgama

**UNHCR na DRC**



# Bustani za tundu la funguo kuboresha mlo katika kambi za wakimbizi

VENANCIA Nibitanga anaonekana akitokea nyuma ya nyumba yake akiwa na fungu la mboga za majani mkononi. Venancia ni miongoni mwa wakimbizi wanaoishi ndani ya kambi ya wakimbizi ya Nduta iliyopo wiliyani Kibondo mkoani Kigoma. Kabla ya kukatakata mboga na kuzipika, huziosha na maji safi ili kutoa mchanga na kisha kuandaa mlo wa familia. Wakati akiendelea na kazi ya kuandaa mboga binti yake mdogo anamwangalia kwa makini. "Nadhani akiwa mkubwa atakuwa mpishi mzuri kama mama yake" anasema Venancia na kisha kucheka kwa sauti.

Venancia alikimbia kutoka Burundi mwezi Aprili 2016 baada ya mumewe kumfanyia vitendo vya Ukatili visivyovumilika. "Mume wangu alizidi kuwa mtu mwenye hasira na asiyejali baada ya machafuko ya kisiasa ya mwaka 2015. Siku moja niliamka na kuchukua Watoto na kukimbilia nao nchini Tanzania. Sikuondoka Burundi na kitu chochote zaidi ya nguo chache tulizoweza kubeba mgongoni." Baada ya safari ya tabu ya takribani siku tatu, Venancia na wanae walifika katika mipaka ya Tanzania wakiwa wamechoka sana na wagonjwa. Hakuna kitu chochote ambacho nakitamani au nakifiria ambacho nilikiacha Burundi mbali na Maisha ya dhiki niliyokuwa nayo" anasema

Venancia anafurahia kuwa miongoni mwa familia 1,300 za wakimbizi ambao wamechaguliwa kuwa wanufaika wa mradi wa bustani za tundu la funguo ambao unalenga kuboresha upatikanaji wa chakula na kuongeza virutubisho. Kupitia mradi huu, Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) kwa kushirikiana na Danish Refugee Council (DRC) wamekuwa wakizisaidia familia zinazochaguliwa na Jamii ya wakimbizi kupitia mikutano ya wazi kuanzisha bustani za tundu la funguo kwa kuwapa mbegu, vifaa na elimu ya uzalishaji wa mboga mboga.

Bustani za tundu la funguo hutengenezwa na vitu mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira ikiwemo masalia ya jikoni, pasipo kuharibu mazigira. Utofauti wa bustani za jikoni na bustani nyingine za kawaida, bustani hizi za tundu la funguo zinahitaji nguvu kidogo, kitendo ambacho huzifanya ziwe bustani pendwa kwa watu wenye umri mkubwa, watoto na hata wale wanaosumbuliwa na maradhi. Lakini pia zinatumia maji kidogo, hazihitaji mbolea wala viwatilifu katika kuazalisha. Faida nyingine ya bustani za tundu la funguo Ni kwamba zina uwezo wa kuzalisha mwaka mzima hata wakati wa kiangazi, na inaweza kuoteshwa aina tano tofauti za mboga kwa wakati mmoja na hivyo kuzipa familia uhuru wa kula mboga za majani tofauti kila siku. Pia bustani hizi zina uwezo wa kuzalisha mboga zinazoweza kulisha familia yenye watu nane.

Kabla ya kuanzishwa kwa mradi huu, Venancia mwenye umri wa miaka 35 alitegemea mgao wa chakula ili kuweza kuilisha familia yake yenye watoto saba kama ilivyo desturi katika kambi za wakimbizi hapa Tanzania. "Tunashukuru kwa chakula ambacho tunagawiwa lakini hakitoshi na hakina mboga za majani" amesema. "Watoto walikuwa wanapata mlo moja kwa siku na tulilazimika kubania chakula ili kiweze kutosha kwa mwezi lakini sasa angalau tuna chakula cha kutosha kutokana na bustani yetu ya Tundu la funguo" aliongeza na kutabasamu.

Mgao wa chakula katika kambi za wakimbizi umepunguzwa siku za hivi karibuni na kufikia aslimia 72 ya Mahitaji ya chakula kwa mwezi. Kupungua kwa kiasi cha chakula ambacho kila familia inapokea kwa mwezi kunatokana na changamoto za gharama za usafirishaji zilizoongezeka kufuatia mlipuko wa Ugonjwa wa virusi vya COVID-19 duniani. Kiasi cha dola za kimarekani milioni 21 zinahitajika ili kuwezesha mgao wa chakula katika kambi za wakimbizi kurejea asilimia 100 katika kipindi hiki na hadi kufikia mwezi Machi 2021.

Baada ya kushuhudia mafanikio ya mradi huu ninataka na wenzangu nao wafaidike. "Mwanzoni nilikuwa nikigawia majirani mboga za majani kutoka kwenye bustani yangu lakini sasa nawafundisha ili na wao waweze kuanzisha bustani zao za tundu la funguo na kujitegemea. Ni rahisi na kila mmoja anaweza kufanya kazi hii ya bustani za tundu la funguo" amesema

Kutokana na ukosefu wa fursa za uzalishaji katika kambi za wakimbizi hapa nchini, wakimbizi hulazimika kutegemea misaada ya kibinadamu kwa kila huduma muhimu ikiwepo chakula na afya. Miradi kama hii ni muhimu katika kuhakikisha kwamba wakimbizi kama Venancia na wengine wapatao 240,000 wanaoishi katika kambi za wakimbizi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeli mkoani Kigoma wanapata nafasi ya kuchangia upatikanaji wa chakula bora na salama kwa familia.



PICHA: UNHCR

# Ufugaji sungura umeboresha upatikanaji wa chakula bora katika kijiji cha Mgama

**UNICEF, CUAMM na TAHEA**

KIJIJ cha Mgama kilichopo halmashauri ya wilaya ya Iringa, ni mashuhuri kwa kilimo cha mazao ya chakula ambayo husafirishwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania. Kijiji hichi kina idadi kubwa ya watoto walio chini ya miaka mitano (725) kuliko vijiji vingine vilivyopo katika kata ya Mgama. Kaya nyingi zilizopo kijiji cha Mgama hazina uhakika wa chakula kutokana na kutopatikana kwa chakula wakati wote.

Katika juhudi za kutoa huduma za lishe, mpango unaofadhiliwa na msaada wa serikali ya Ireland umelenga kupunguza udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka miwili mkoani Iringa na Njombe. UNICEF kushirikiana na serikali ya Tanzania pamoja na mashirika ya CUAMM na TAHEA, wanatekeleza mpango wa kuwezesha uzalishaji na upatikanaji wa chakula mbalimbali katika kaya zilizopo mikoa ya Iringa na Njombe.

Sabina Pilla, 54, ni mganikazi anaeishi katika kijiji cha Mgama. Kazi yake ya uganikazi inahusisha kuwa mkulima wa mfano na kutoa elimu ya kilimo na mifugo katika kijiji anachoishi. Sabina ni kati ya waganikazi 96 kutoka mkoa wa Iringa waliopata mafunzo ya kilimo bora na ufugaji wa wanyama wadogowadogo. Mwaka 2018, alihamasisha jamii kuanzisha kikundi cha uhasihi kwa ajili ya kujifunza kuhusu Kilimo na ufugaji bora. Kikundi kiliitwa "Mtoto Kwanza" chenye idadi ya wanakikundi 25. Kikundi kilihamasishwa kuanzisha bustani za nyumbani na ufugaji wa sungura.

Katika juhudi za kutoa huduma za lishe, waganikazi wote 96 walipewa sungura wawili kwa lengo la kuwafunga wazaliane na kuwagawia walengwa wa mradi ambao ni wajawazito na kina mama/walezi wenye watoto wa umri chini ya miaka 2. Baada ya miezi 4, Sabina alikua na sungura 20 ambapo aligawa sungura 16 katika kaya 8 zilizipo katika kikundi cha "Mtoto Kwanza". Wanakikundi 8 waliopata sungura waliendelea kufuga na kuwagawia wengine na mzunguko ukaendelea.



Kufikia Septemba 2018, kaya 56 zenye watoto zilizopo kijiji cha Mgama na kijiji cha karibu cha Ibumila zimenufanika kupata jumla ya sungura 112. Kaya 72 zilizopo katika mpango wa kupata sungura, zimeweza kuanzisha bustani za nyumbani ili kuweza kupata virutubishi vingine vilivyopo katika mbogamboga mbalilmbali. Katika mpango huu wa kugawiana sungura, kaya zilihamasishwa kuuza sungura wachache na kula wengine ili kuongeza upatikanaji na ulaji wa vyakula venye protini. Fedha iliyopatikana kutokana na mauzo ya sungura, zimetumika katika kununua mbolea kwa ajili ya kilimo cha mahindi na nyanya. Pia, mbolea ya sungura inatumika bustani za nyumbani na katika uzalishaji uyoga.

Agnes Kitime, 35, anaishi na mume wake pamoja na familia yenye watoto wanne. Agnes anaishi jirani na Sabina na pia ni mwenyekiti wa kikundi cha "Mtoto Kwanza". Baada ya kuhamasishwa, Agnes aliweza kufuga sungura wengi na kuanzisha bustani nyumbani kwake. Juhudi zake zilipelekea kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa kikundi. Pamoja na faida nyingine, Agnes ameweza kupangilia chakula na lishe bora katika familia yake. Baada ya kufanikiwa, Agnes anasema, "Mtoto wangu wa miaka miwili, Oliva Kalinga anapata chakula chenye lishe mchanganyiko na ameweza kukua vizuri. Anapata chakula chenye protini kinachomwezesha kukua vizuri kimwili na kiakili."

Agnes aliendelea kusema, "Mimi pamoja na familia yangu hatukuwahi kula nyama ya sungura kabla ya mpango huu kuanza, pia sikuamini kama uzalishaji wa sungura unaweza kukuongezea kipato. Lakini kupitia kikundi chetu cha unasihi, nilijua kwamba nyama ya sungura ni tamu na nzuri kwa afya hasa kwa mtoto wangu Oliva. Watoto wangu wote sasa wanapenda sana nyama ya sungura na wamekua wakinikumbusha niwapikie nyama ya sungura."

## Kutafuta ufumbuzi wa mahalia kukabili lishe duni Tanzania

**Vincent Browne na Alice Maro**

WAKATI Joyce Mihinzo, ambaye ni mama wa watoto wa kiume wawili, alipojiunga na mradi wa Boresha Lishe, tayari alikuwa na mimba changa. Mradi huo unafadhiliwa kwa ushirikiano katii ya Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Japan na kutekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniai (WFP) katika mikoa ya Dodoma na Singida nchini Tanzania. Kupitia mradi huo, Joyce alipata matibabu na unga wa uji ulioongezewa virutubisho, Super Cereal, kwani alikuwa akisumbuliwa na Utapiamlo. Vilevile, alipata ushauri wa lishe kuhusu vyakula bora zaidi vya kula wakati wa ujauzito na pia vidokezo kuhusu namna ya kuilisha familia yake.

Msaada huu kupitia mradi wa Boresha Lishe, pamoja na mahudhurio ya mara kwa mara katika kituo cha afya ili kuchunguza afya, vilimsaidia kuvuka salama awamu za kwanza na pili za ujauzito wake. Hata hivyo, katika awamu ya tatu, yaani miezi mitatu ya mwisho, alipatwa na dharua wakati alipokuwa safarini kutembelea ndugu zake walio mjini, na hasa kwa sababu alikuwa mbali na kituo chake cha afya cha kufanyia uangalizi wa ujauzito wake. Hivyo, alijifungua mtoto wa kike njiti wakati mimba ina umri wa miezi saba tu. Mtoto huyo alikuwa na uzito wa kilo 2.3. Kwa kuwa alikwishapatiwa mafunzo, Joyce aliweza mara moja kuanza kumnyonyesha mtoto wake mchanga akihakikisha yeye na mtoto wanapata lishe muhimu ili yeye apone vizuri na mtoto akue vizuri.

Kutokana na Tamari kuzaliwa njiti, Joyce aliendelea kuhakikisha anakula uji ule ulioongezewa virutubisho katika mlo wake wa kila siku, jambo lililomsaidia kutoa maziwa yenye ubora yaliyokidhi maridhawa mahitaji ya chakula ya mtoto. Yeye na mtoto waliporuhusiwa kurudi nyumbani kutoka hospitali, Joyce aliendelea kutumia uji ule ulioongezewa virutubisho. Mara Tamari alipokuwa na umri wa miezi sita, alikuwa tayari amekomaa vya kutosha kuweza kulishwa uji huo moja kwa moja. Joyce pia aliendelea kupokea msaada kutoka katika mradi wa Boresha Lishe katika muundo wa huduma za afya za baada ya kujifungua, ushauri kuhusu lishe, kusaidiwa kuendesha bustani ya mbogamboga nyumbani ili kuhamasisha kilimo cha mbogamboga tofautitofauti kuimarisha mtawanyiko wa lishe kamili, na maelekezo kuhusu tabia njema katika maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi (WASH).

Akina mama kama Joyce—wanaopata mlo ulioongezewa virutubisho unaotoka mahali wanakoishi ulio na ufanisi na wa gharama nafuu linaweza kuwa jambo la kufa na kupona. Moja ya vikwazo vikubwa katika kukabiliana na utapiamlo katika umri wa utoto nchini Tanzania ni kukosekana kwa vyakula vya nyongeza vyenye gharama nafuu, vinavyopatikana mahalia na vinavyoendana na utamaduni. Ili kuwasaidia akina mama vizuri, WFP inashirikiana na wazalishaji wenyeji wa vyakula vya nyongeza vyenye virutubisho maalumu. Mwezi Agosti, mwaka huu, Kituo cha Chakula na Lishe cha Tanzania (Tanzania Food and Nutrition Centre) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba cha Muhimbili, Shirika la Viwango la Tanzania, kwa msaada wa kiufundi kutoka WFP, EU vilizindua mradi wa kusaidia kuzuia utapiamlo kwa watoto wenye umri wa kati ya miezi 6 na miaka 5 nchini Tanzania. Mpango huu ambao umeanzishwa kama sehemu ya mradi wa Boresha Lishe unalenga kupata ufumbuzi muhimu wa hapa nchini kwa janga la lishe duni.

Mradi huo unajumuisha utayarishaji wa vyakula vya nyongeza na ziada (ready-to-use complementary and supplementary foods (RUFs)) ili kukabiliana na kudumaa na kwa ajili ya kutibu tatizo la utapiamlo mkali. Bidhaa hizi zitaandaliwa kutokana na viungo vinavyopatikana mahalia, yaani vile vilivyozoeleka katika milo ya kila siku, vitakavyoandaliwa ili kukidhi viwango vya ubora na usalama wa lishe vinavyotakiwa.

Licha ya hilo, mradi huo pia unaweka vipimo na viwango vya uzalishaji unaofanywa na wenyeji wa vyakula maalumu vya lishe. Jambo hili linawapa nafasi wajasiriamali na wazalishaji wa vyakula wa nchini Tanzania kuzalisha bidhaa zao wenyewe, hivyo kuongeza upatikanaji wa vyakula vyenye lishe nchini Tanzania. Ushirikiano huu pia unatoa fursa ya kuimarisha Lengo la UN la 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG-17) la kujenga ushirika kati ya taasisi binafsi na za umma pamoja na vyuo vikuu na serikali ili kupanua masuala ya lishe, na hivyo kushirikiana katika kufikia Lengo la 2 la UN la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG-2)—Kumaliza Njaa. Kwa hiyo, siyo tu kwamba mradi huu unasaidia Tanzania kuimarisha lishe, bali pia una manufaa ya kiuchumi kwa nchi katika muda wa kati na mrefu.

***Waandishi wa makala hii ni Maafisa Mawasiliano WFP Tanzania***



PICHA: FAO/DANIEL HAYDUK

# Kutokomeza utapiamlo iko ndani ya uwezo wetu

Na Charles Tulahi

TAARIFA zilizopo zinaonyesha kwamba viwango vya udumavu vimepungua kwa asilimia 3.2 tangu mwaka 2012. Uzalishaji wa chakula unastawi nchini, huku mikoa kama vile Mbeya, Rukwa, na Ruvuma ikizalisha chakula zaidi ya asilimia 40 kuliko vile ambavyo watu wake wanahitaji.

Takwimu hizi na nyingine zinaonyesha mafanikio makubwa ya Tanzania katika muongo uliopita. Cha kushangaza zaidi ni kwamba baadhi ya mikoa iliyo na uzalishaji mkubwa wa chakula ndio mikoa iliyo na viwango vikubwa zaidi vya udumavu. Kukua kwa uchumi pia kumesababisha aina mpya za utapiamlo, kama vile kuongezeka uzito na unene uliopitiliza, ambavyo vinaongezeka, pamoja na magonjwa yasiyoambukiza yanahusiana na lishe.

Ukweli huu wenye taswira ya uwongo ulio wazi unatufundisha kwamba kuongezeka kwa idadi ya watu kunahitaji juhudi kubwa zaidi iwapo tunataka kutokomeza njaa na aina zote za utapiamlo ifikapo 2030. Mambo haya yanatukumbusha kwamba kuzalisha chakula kingi zaidi hakupunguzi mara moja utapiamlo au udumavu. Bali huweka msisitizo juu ya haja ya sio tu kuwalisha watu, bali pia kuwapatia lishe yenye afya kwa wote.

Ripoti ya hivi karibuni ya Programu ya Matokeo juu ya Usalama wa Chakula na Lishe, Ustahimilivu, Uendelevu na Mageuzi (FIRST) - ikiwa ni ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Umoja wa Ulaya - ili kuboresha sera katika nyanja za uhakika wa chakula na lishe, unasisitiza umuhimu wa kuwekeza katika lishe zenye afya.

Mabadiliko ya tabia nchi na mitikisiko mingine inaonekana pia kuwa na athari hasi kwenye uhakika wa chakula na lishe. Kati ya mwaka 1961 na 2016, wastani wa halijoto kwa kila mwezi nchini uliongezeka kwa nyuzijoto 0.6 Celsius, na mvua zilipungua kwa milimita 6.4. Mabadiliko haya yameelekea kudhoofisha uzalishaji wa chakulana kufanya hali ya magonjwa na wadudu waharibifu kuwa mbaya zaidi, wadudu kama vile Viwavi Jeshi na wengineo.

Hivyo basi ni muhimu sana kuwekeza katika mifumo inayopunguza wepesi wa kuathirika kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wanaokabiliwa na changamoto za dhahiri na kuwasaidia katika kubadilika ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ripoti hiyo inasisitiza. Ripoti pia inahimiza kuongeza nguvu katika afua zinazolenga katika kujenga ustahimilivu wa tabianchi na kujenga mazingira wezeshi yanayovutia uwekezaji (kuanzia wakulima wadogo hadi viwanda vikubwa vya kilimo). Kuendeleza na kukuza matumizi ya teknolojia za kilimo zinazofaa ambazo zinamudu mabadiliko ya tabia nchi katika kanda zote za kiekolojia ya kilimo, haya ni mojawapo ya mambo mengi yenye matumaini ambayo unaweza kuchagua.

Kupitia uchambuzi wa kitafiti, pamoja na mashauriano mapana na wadau muhimu katika sekta za chakula na lishe, ripoti hii imeainisha njia kuu tatu za kuharakisha maendeleo:

Kwanza, kilimo cha Tanzania kinachokua kwa kasi kinatoa uwezekano mzuri wa kuchangia kutokomeza utapiamlo kupitia mbinu zinazojali zaidi lishe. Licha ya upatikanaji wa chakula, hatua za makusudi ambazo zinalenga katika uanuwai wa lishe na usalama wa chakula kwa wote, zitakuwa na matokeo chanya ya kudumu katika maendeleo ya rasilimali watu. Kuongeza uzalishaji na ulaji wa bidhaa zenye virutubisho vingi kama vile matunda, mboga mboga, mikunde na karanga, samaki na bidhaa za mifugo, zina matokeo makubwa sana katika kupunguza utapiamlo.

> Programu za mafunzo zilizoboreshwa kuhusiana na kilimo na lishe kwa wataalamu wa lishe na kilimo, kuimarisha uratibu baina ya sekta za afya na kilimo kutaimarisha mapambano dhidi ya utapiamlo.

Kwa mantiki hiyo basi, kampeni za kuinua ufahamu juu ya umuhimu wa uanuwai wa lishe utasaidia walaji kuchagua lishe iliyo na afya zaidi na kutuma ujumbe sahihi kwa wakulima, watu wa mauzo na watendaji wengine katika mnyororo wa thamani wa chakula, na kutumia utendaji unaoziunganisha vizuri zaidi sekta za kilimo na lishe.

Pili, programu za mafunzo zilizoboreshwa kuhusiana na kilimo na lishe kwa wataalamu wa lishe na kilimo, kuimarisha uratibu baina ya sekta za afya na kilimo kutaimarisha mapambano dhidi ya utapiamlo.

Mwisho, ni kazi kidogo sana inayoweza kufanyika bila ya rasilimali. Pamoja na umuhimu wake, kilimo kinahitaji uwekezaji mkubwa kwa ajili ya afua zinazojali lishe. Kupambanua uwekezaji kwa ajili ya sekta ya kilimo (hususani kwa utafiti ya jinsi kilimo kinaweza kusaidia kuzuia magonjwa yasiyoambukiza, kukabiliana na tishio la mabadiliko ya tabia nchi) kutoa ahadi na kuhamasisha rasilimali za ziada ni baadhi ya sera bora unazoweza kuchagua. Ukichukulia kwamba Tanzania imeingia katika hadhi ya uchumi wa kati, uwekezaji mkubwa wa makusudi hauna budi kufanyika katika maendeleo ya rasilimali watu ili kurudisha nyuma viwango vya udumavu vilivyopo, ambavyo vinalemaza uwezo wa kimwili na utambuzi wa kundi kubwa la watoto chini ya umri wa miaka mitano.



PICHA: FAO/DANIEL HAYDUK

Pakiwa na vipaumbele vingi vinavyoshindana pamoja na mwitikio baada ya gonjwa la Covid 19, kamwe fedha za umma haziwezi kutosheleza. Wabia wa maendeleo, Asasi za Kiraia (AZAKi), sekta binafsi, na wadau wengine wenye nia njema wanahitaji kushiriki na kujihusisha katika ajenda ya lishe, iwapo tunataka tusiache hata mtu mmoja nyuma ifikapo mwaka 2030. Lishe na afya ni mambo yanayomhusu kila mtu. Kila mtu ajiunge; hususani vijana na wanawake, kwani wao ndio wanaoshikilia funguo za mafanikio. Kesho . Kesho Yetu Inajengwa na Lishe Bora Endelevu. Matendo Yetu ndio Mustakabali wetu.



PICHA: IFAD/MWANZO MILINGA

# Kufanya kazi kwa pamoja kubadilisha kilimo vijijini Tanzania

**Na Francesco Maria Rispoli**

NJAA inaongezeka. Mwaka 2019, karibu watu milioni 690 walilala na njaa na athari za janga la COVID-19 zinavuruga mifumo ya chakula duniani kote. Wakati dunia inaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Chakula Duniani tarehe 16 Oktoba 2020, ni wakati wa kutafakari jinsi tunavyoweza kurudi kwenye njia ya kufanikisha kuwa na dunia isiyo na njaa.

Dhamira ya mwaka huu, "Kesho Njema Inajengwa na Lishe Bora Endelevu," inaendana na agizo la IFAD la kuwekeza vijijini ili kupunguza umaskini, kuongeza usalama wa chakula, kuboresha lishe na kuimarisha uthabiti kupitia kilimo.

Kilimo sio tu muhimu katika uzalishaji wa chakula bali pia hutengeneza ajira, huzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda na kuleta mapato ya fedha za kigeni. Kilimo kinachangia asilimia 31 ya Pato la Taifa (GDP), kinachangia hadi asilimia 24.9 ya mapato ya nje na kuajiri watu karibu milioni 37 nchini Tanzania.

IFAD inatambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta ya kilimo na msaada inaotoa kwa serikali ya Tanzania katika kuendeleza kilimo na kubadilisha maeneo ya vijijini. Hadi sasa uwekezaji wa IFAD wa dola za Kimarekani milioni 430 umezifikia zaidi ya kaya milioni 4 za vijijini nchini Tanzania.

> "Lishe bora ni moja ya vipaumbele muhimu vya maendeleo ambavyo Tanzania imedhamiria kufikia ifikapo mwaka 2030 chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Takribani asilimia 80 ya uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini unatokana na wakulima wadogo wadogo. Wakulima hawa wana jukumu muhimu la kuwalisha watu wa maeneo yao na kuendeleza uchumi wa vijijini. Hata hivyo, wengi wao bado wanategemea kilimo cha mkono na uzalishaji unaotegemea mvua. Hii imewafanya wawe katika hatari kubwa ya mtikisiko - kutoka kwa hali ya hewa au dharura zingine.

Wakulima wadogo wadogo wapo katika kitovu cha miradi inayofadhiliwa na IFAD. Sio tu kwamba wao ni miongoni mwa wanufaika wakuu lakini kazi na maarifa yao yanatoa michango muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu ya miradi. IFAD imesaidia miradi 15 nchini Tanzania ambayo lengo lake limekuwa kuongeza tija na faida kupitia utoaji wa pembejeo za kilimo, msaada wa ugani na kutumia mbinu nzuri za kilimo.

Wakulima wa Magu, Kagera na Zanzibar ni baadhi ya wanufaika wa uwekezaji huo. Chini ya Miundombinu ya Masoko, Nyongeza ya thamani na mpango wa kusaidia Kifedha Vijijini, uzalishaji wa mpunga unaofanywa na wakulima wadogo umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, mavuno ya mpunga yameongezeka kwa asilimia 150 huko Magu, mavuno ya mahindi kwa asilimia 350 mkoani Kagera na mavuno ya nyanya kwa asilimia 200 visiwani Zanzibar. Kwa wakulima wengi wadogo wadogo ongezeko hilo kubwa la mavuno hujenga fursa za kibiashara, na kuwawezesha kuinua kipato chao na kuwekeza katika teknolojia ya kisasa.

Mapato makubwa pia hutumika kununua chakula chenye virutubisho zaidi, na kadri mashamba yanavyokuwa na tija zaidi, tunashirikiana nao kuboresha ubora wa lishe ya mazao yao. Lishe bora ni moja ya vipaumbele muhimu vya maendeleo ambavyo Tanzania imedhamiria kufikia ifikapo mwaka 2030 chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Utafiti unaonesha kuwa utapiamlo husababisha matatizo ya kiafya na hasara katika uzalishaji wa kiuchumi. Bila upatikanaji wa chakula cha kutosha, cha bei nafuu, chenye virutubisho, vizazi vinaendelea kunaswa katika umaskini, kushindwa kutumia fursa za elimu na kazi kutimiza uwezo wao. Kuwekeza katika lishe kupitia kilimo sio tu kuwajibika kijamii bali maendeleo makubwa na uchumi mzuri.

Visiwani Zanzibar, IFAD imesaidia uzalishaji wa bidhaa bora za chakula kwa watoto kupitia Chama cha Ushirika cha Mboga Mboga Tungalipo ambacho husambaza ndizi na mbogamboga kwenye shule za jirani. Hii imeongeza ulaji wa vitamini kwa watoto wa shule.

Mafanikio ya IFAD nchini Tanzania kwa miaka mingi yanaweza kuhusishwa na ushirikiano mkubwa na Serikali. Kimsingi, ngazi mbalimbali za serikali zimeendeleza mbinu za mafanikio ya miradi inafadhiliwa na IFAD. Umiliki huu unaenea kwa taasisi nyingine kama mashirika ya wakulima na sekta binafsi.

Soko la Kinyasini huko Unguja ni mfano wa jinsi umiliki wa serikali una matokeo endelevu ya miradi. Soko lilijengwa mwaka 2017 na kupewa vifaa vya chumba cha baridi kwa ajili ya mbogamboga, matunda na samaki. Tangu lilipokabidhiwa kwa halmashauri ya wilaya hiyo mwaka 2018, soko hilo limewanufaisha wafanyabiashara 350 wanaouza mazao mbalimbali ya kilimo kwa wananchi wa maeneo hayo na ukanda wa hoteli za kitalii. Hii imebadilisha maisha yao na kusaidia kujenga uthabiti wa mfumo wa chakula wa eneo hilo.

Ili kila kitu kiwe pamoja, ushirikiano ni kiini cha kazi ya IFAD. Tunafanya kazi kwa kushirikiana na wananchi wa vijijini, serikali, mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, washirika wa maendeleo na sekta binafsi kwa lengo la pamoja la kubadilisha kilimo vijijini Tanzania kuendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 na Mipango ya Maendeleo ya Taifa Tanzania.

Kufanya kazi kwa pamoja kuelekea malengo haya sio tu kunaboresha ufanisi wa miradi lakini pia kunatuwezesha kuwafikia watu wengi zaidi na kuwa na matokeo makubwa nchini. Ushirikiano wetu na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa ya Roma kama Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) na Mpango wa Chakula Duniani (WFP) umehakikisha mamilioni ya Watanzania hawalali na njaa.

Ikiwa imebaki miaka kumi kuelekea mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, muda wa kuchukua hatua ni sasa! IFAD inathibitisha tena dhamira yake ya kutokuwa na njaa ifikapo 2030. Jiunge nasi tunawezesha jambo hili kutokea.





# Jiji laja na mpango mpya kudhibiti uchafuzi mazingira

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imebuni mbinu mpya ya kukabiliana na watu wanaochafua mazingira kwa kuwaweka askari kanzu (mgambo) kila mahali kuwakamata wanaotupa taka ovyo.

Hatua hiyo imetokana na baadhi ya wananchi kutupa taka ovyo licha ya kuwapo kwa vyombo vya kuhifadhia taka katika maeneo mbalimbali.

Ofisa wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Jiji, Ali Mfinanga, alisema wameandaa sheria ndogo ambazo zitasimamiwa na askari hao ili kudhibiti hali hiyo.

Mfinanga alisema ili kulifanya jiji kuwa safi, wameandaa mpango kabambe wa kuhakikisha kunakuwa na askari hao kwenye maeneo yote kwa ajili ya kuwadhibiti wale ambao wanakiuka sheria za utunzaji wa mazingira.

"Tuna Kampuni ya Green West ambayo kazi yake ni kufanya usafi, lakini ili kuwadhibiti wale ambao si watekelezaji wa sheria, tunakuja na mpango wa kuwa na mgambo kwenye maeneo yote kama ilivyo Manispaa ya Moshi," alisema Mfinanga.

Kaimu Meneja wa Green West Dodoma, Sebastian Mkomagi, alisema kampuni hiyo imekuwa ikimuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, katika utunzaji wa mazingira, hivyo ni vyema Watanzania wakaishi kwenye misingi hiyo.

Pia alisema kila mtu anatakiwa kumuenzi Baba wa Taifa kwa kutunza mazingira, kufanya usafi na upandaji wa miti.

Mmoja wa waliofanya usafi Kata ya Uhuru ikiwa ni kumbukumbu ya kifo cha Nyerere, Mlimbwende wa Utalii Mkoa wa Dodoma nafasi ya tatu 2020 (Miss Tourism Dodoma), Dorice Mhagama, aliliomba jiji kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira ikiwa ni njia mojawapo ya kudhibiti taka ngumu kuzagaa ovyo.

"Kwenye mitaro kumekuwa na taka ngumu. Hii inasababishwa na baadhi ya watu pengine kutokuwa na elimu na madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira na wengine kukaidi," alisema. "Sasa elimu itolewe na kuwapo mgambo kwenye maeneo yote wa kuwawajibisha na kuwaelekeza wananchi kama ilivyo Moshi, hapo mazingira yatakuwa safi wakati wote," aliongeza.




Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi wa kitengo cha Kanisa la Free Pentecostal of Tanzania (FPCT), Wilaya ya Bahi jijini Dodoma, Janne Mgidange, akizungumza na wazazi na walezi kwenye ufunguzi wa uanzishaji wa baraza la watoto wenye ulemavu, jijini humo jana.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watoto watoa neno uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

BARAZA la Watoto Wenye Ulemavu Dodoma Mjini, limewaomba Watanzania wenye sifa ya kupiga kura kuhakikisha wanachagua viongozi watakaolinda na kutetea haki zao za msingi.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lisia Kusaduka, alitoa ombi hilo alipokuwa akitoa shukrani zake kwa niaba ya watoto wenye ulemavu kwa serikali na Kanisa la The Free Pentecostal of Tanzania (FPCT) chini ya kitengo cha mradi wa elimu jumuishi kwa uanzishaji wa baraza wilayani Dodoma.

Kusaduka aliwaomba wenye sifa za kupiga kura kujitokeza Oktoba 28, mwaka huu, kuwachagua viongozi watakaowapa haki zao za msingi ya kila siku bila kubaguliwa. Alitaja baadhi ya haki hizo ni pamoja na elimu, matibabu, ulinzi, uwakilishi kwenye maamuzi, na kutambuliwa kwenye fursa za ajira bila kubaguliwa.

Kadhalika, aliomba serikali kuchukua hatua kali kwa baadhi ya wazazi na jamii ambao wanaoendelea kuwaficha kwa kuwafungia watoto wenye ulemavu nyumbani bila kujali utu wao.

Alisema kitendo hicho ni cha ukatili kwa kuwa kinaongeza umaskini kwa mtoto huyo ambaye amegeuzwa kama mfugo unaofungiwa ndani ya zizi, pia kinamnyima kupata haki zake za kimsingi kama wengine ambao hawana ulemavu.

"Sisi Baraza la Watoto wenye ulemavu, tunaiomba serikali yetu sikivu kutowafumbia wazazi,walezi na hata na baadhi ya makabila ambayo bado yana mtizamo hasi wa kufikiri kuwa motto mwenye ulemavu ni mkosi kwa upande wao," alisema.

Mwenyekiti huyo aliwataka watoto ambao wapo shuleni kuhakikisha wanajibidiisha kielimu zaidi ili kuondokana na vikwazo vinavyowakabili. Awali, akitoa ufafanuzi wa kuundwa kwa baraza hilo, Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi Wilaya za Bahi na Dodoma, ambao uko chini ya kitengo cha FPCT, Jane Mgidange, alisema kuwa bado kuna tatizo baadhi ya wazazi, walezi na jamii kuwachukuliwa watoto hao kama mifugo na kulazimika kuwafungia ndani.

Ofisa huyo alisema kuwa mradi huo upo kwa ajili ya kuwatambua watoto wenye ulemavu ili upatiwa misaada mbalimbali, ili kumudu maisha yao hivyo hakuna sababu ya kuendelea kuwafungia ndani kama mifugo. Naye Ofisa Elimu Msingi Jiji la Dodoma, Joseph Madeyo, alisema serikali kamwe haitakaa kimya kuona watoto wenye ulemavu wakikosa haki zao za kimsingi kama ilivyo kwa wengine ambao hawana ulemavu.

Alisema serikali itaendelea kuwathamini na kuwatambua watoto hao wenye ulemavu ili kujengewa miundombinu rafiki itakayowawezesha kupata mahitaji yao kama vile kwa upande wa elimu, afya na vifaa saidizi.

# Wanafunzi watakiwa kupaza sauti ukatili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI wa kike wametakiwa kupaza sauti zao wanapofanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kulazimishwa kuolewa wakiwa na umri mdogo na hivyo kukosa fursa ya kuendelea na masomo yao.

Ofisa Jamii wa Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), Asha Ramadhani, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na utu wa mtoto.

Alisema watoto hao wana haki ya kufikia malengo yao, hivyo wana wajibu wa kupaza sauti ili kukomesha vitendo hivyo.

Ramadhani alieleza CDF wanaelimisha watoto kujitambua katika nyanja mbalimbali ili kufikia malengo yao.

Alisema Jukwaa hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Action Girls Foundation, wamekuwa wakifanya makongamano ambayo husaidia kuwakumbusha watoto na wazazi umuhimu wa mtoto wa kike.

Mmoja wa wanafunzi, Kuluthumu Iddi, alisema kutokana na elimu inayoendelea kutolea na mashirika mbalimbali ya utetezi wa watoto vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike vimepungua.

"Watoto wa kike hata wale wa vijijini wameanza kutambua haki zao, wasichana wengi sasa wanakwenda shuleni, serikali iongeze juhudi zaidi katika kupambana na vitendo vya kikatili, mashirika ya utetezi wa watoto yanasaidia sana kubadilisha fikra za sisi wasichana tuliopo shuleni kwani elimu tunayopata inaenda kusaidia jamii inayotuzunguka," alisema.

Mwanafunzi Sophia Mwasamila kutoka Shule ya Sekondari ya Mazae, alisema watoto hao wamekuwa wakikumbana na vikwazo vingi ikiwamo kulazimishwa kuingia katika ndoa kabla ya wakati.

Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa Taasisi ya Action Girl Foundation, Rabia Sady, alisema wazazi wanapaswa kuheshimu watoto wa kike na sio kuwatoa shule wakati wanahitaji kutimiza ndoto zao.

Alisema elimu ya uzazi kwa vijana wa rika balehe waliopo shuleni ni muhimu kutokana na kwamba wanapaswa kuijua na wazazi wanapaswa kuwaelimisha watoto.



HABARI MBEYA

# Bosi wa TCRA ahimiza vijana uchumi kidigitali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Asajile John, amewataka vijana kutumia vyema teknolojia za mawasiliano hususani TEHAMA katika shughuli za uzalishaji, ili kulisaidia taifa kufikia uchumi wa kidigitali.

Asajile alitoa rai hiyo juzi wakati wa kongamano lilowahusisha vijana wa shule za sekondari na vyuo kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kwenye Siku ya Kumbukizi ya Kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, lililoandaliwa na Shirika la Lightness Tanzania.

Alisema vijana wanapaswa kuenzi falsafa ya Hayati Mwalimu Nyerere ya kujitegemea kwa kuhakikisha wanatumia teknolojia za mawasiliano kujiletea maendeleo ikiwa ni pamoja na kutumia kwenye shughuli za biashara, kilimo na wanafunzi kujisomea na kutafuta ajira.

"Kifo cha Mwalimu Nyerere kinatukumbusha Watanzania kuyaenzi na kuyafanya yale aliyoyaagiza kama vile falsafa ya uhuru wa kujitegemea kwa kuhimiza watu waendelee kufanya kazi kwa bidii na alijitahidi kuboresha miundombinu ya mawasiliano katika kila pembe ya nchi," alisema.

Asajile alisema lengo la TCRA ni kuhamasisha vijana kutumia kwa manufaa yao kama vile kufahamu mabadiliko mbalimbali yanatokea duniani na kuwa makini na matumizi ya TEHAMA ili kujiepusha na uvunjifu wa sheria za mitandao.

Akifungua kongamano hilo, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA) Tawi la Mbeya, Dietrich Mgaya, alipongeza awamu mbalimbali za uongozi wa nchi kwa kuendelea kuziishi falsafa za Hayati Mwalimu Nyerere kwa kutoa huduma bora za jamii katika masuala ya afya, elimu, umeme na maji.

Sambamba na hayo, Mgaya pia aliwapongeza viongozi hao kwa kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za umma pamoja na kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Mkurugenzi wa Shirika la Lightness Tanzania Organization, Aliko Brown, alisema wanajihusisha na shughuli za kuongeza maarifa kwa jamii na kuwahamasisha waendelee kujitegemea kwa kubuni na kuanzisha shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato. Alisema falsafa ya uhuru wa kujitegemea kama ajenda yao katika kumuenzi Mwalimu Nyerere, inawakumbusha vijana kujiamini, kuwa wabunifu na kufanya utafiti ili ulete tija kwa taifa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari St. Marry's, Cornelius Mtambo, alisema moja ya jukumu walilonalo ni kuwaandaa wanafunzi kujitegemea kabla na baada ya kumaliza masomo yao.

# Mtafiti aanika maajabu uji wa ulezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTAFITI wa Mazao ya Nafaka wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Denis Tippe, amebainisha maajabu ya uji wa ulezi katika kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto.

Dk. Tippe aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa juzi kuwa uji wa ulezi una virutubisho na madini mengi, yakiwamo ya zinki, ambavyo vinasaidia kukabiliana na udumavu, hivyo akashauri wananchi kutumia uji huo.

Alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa vyakula, lakini inaongoza kwa udumavu wa watoto kutokana na utamaduni wa wananchi kwenye ulaji ambao hauzingatii chakula bora.

Alisema uji wa ulezi ndiyo utakuwa suluhisho la tatizo hilo ikiwa wananchi wakiutumia pamoja na vyakula vingine vinavyotokana na ulezi.

"Kwa sasa tupo kwenye maadhimisho ya Wiki ya Lishe Duniani, ukifuatilia takwimu, zinaonyesha mikoa yetu ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwenye uzalishaji wa chakula, lakini inaongoza kwa tatizo la udumavu na sasa hivi inaonyesha tatizo liko zaidi ya asilimia 40," alibainisha.

Dk. Tippe alisema mikoa hiyo ni miongoni mwa mikoa ambayo zao la ulezi linastawi vizuri na hivyo akasisitiza hakuna sababu kuendelea kukabiliwa na tatizo la udumavu.

Alisema mbali na vyakula vitokanavyo na ulezi kusaidia kukabiliana na udumavu, pia vinawasaidia watu wanaougua ugonjwa wa kisukari kwa maelezo kuwa ni miongoni mwa vyakula ambavyo mmeng'enyo wake unachukua muda mrefu tofauti na mazao mengine.

Pia, alisema ulezi una madini ya chuma ambayo yanasaidia kuimarisha mifupa na meno na hivyo kusaidia watu kuwa na mifupa imara na kutong'oka meno mapema. Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kwa sasa taasisi hiyo imeanza utaratibu wa kugawa uji wa ulezi kwa watumishi na wageni wote watakaokuwa wanatembelea taasisi hiyo.

Alisema lengo la kuanzisha utaratibu huo ni kutoa hamasa kwa wananchi kutumia uji huo pamoja na vyakula vingine vinavyotokana na ulezi ikiwamo ugali.

Alisema taasisi hiyo imefanya utafiti wenye lengo la kufufua mazao mbalimbali ya asili ambayo yalikuwa yameanza kupotea ukiwamo na ulezi kwa maelezo kuwa mazao hayo yana viini muhimu ambavyo vinasaidia kwenye afya za watu.

"Ukiacha kuwa ulezi ni chakuala lakini pia ni uchumi, ulezi tulioufanyia utafiti kwenye kituo hiki unaweza kumsaidia mtu kupata mpaka Sh. milioni 16 kwa ekari moja, hivyo tunawashauri wananchi waanze kuchangamkia," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa sasa wanataka kubadili fikra za wananchi kuwa ulezi unalimwa zaidi maeneo yenye ukame ili ulimwe maeneo mengi nchini.



Maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakifanya jaribio la kuuzima moto wakati wa kufunga mafunzo ya miezi mitatu kwa maofisa hao, yaliyofanyika katika Chuo cha Magereza Kiwira, mkoani Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgombea aahidi soko la uhakika wakulima pareto

**Na Nebart Msokwa,**

MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Mbeya Vijijini (CHADEMA), Joseph Mwasote, maarufu China wa China, amesema akichaguliwa kuliwakilisha jimbo hilo bungeni, atahakikisha anawasaidia wakulima wa pareto kupata soko la uhakika.

Alitoa ahadi hiyo juzi katika mkutano wa kampeni Kata ya Ilembo, akisisitiza kuwa kwa sasa zao hilo halina soko la uhakika.

Mwasote alisema baadhi ya wakulima wameanza kukata tamaa na kuacha kulima zao hilo na badala yake wameanza kupanda miti ya mbao pamoja na mazao mengine yakiwamo mahindi na viazi mviringo ambayo ni maarufu kwenye ukanda huo.

Alisema akichaguliwa na wananchi hao, atahakikisha anashirikiana na serikali kutafuta wawekezaji ambao watawekeza viwanda vya kuchakata zao hilo kwenye ukanda wa Umalila ambao zao hilo linazalishwa zaidi ili kuwasogezea soko wananchi.

"Sisi huku ndiyo wakulima wakubwa wa pareto na tunazalisha pareto yenye sumu nyingi, lakini kiwanda kimeenda kuwekwa Mafinga mkoani Iringa na wanunuzi wanapeleka huko, jambo ambalo halitusaidii sisi huku, hivyo ninaombeni kura zenu ili nikapambanie suala hilo," alisema Mwasote.

Alisema mbali na zao hilo, wakulima wa viazi mviringo pia wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa soko la uhakika wa zao hilo kutokana na miundombinu ya barabara kutokuwa rafiki na hivyo akawaahidi wananchi hao kuwachagua wagombea wa CHADEMA.

Alisema serikali ya chama hicho itaboresha miundombinu ya barabara kwenye maeneo yote ya uzalishaji ili kuwarahisishia wananchi usafirishaji wa mazao kutoka kwenye mashamba kwenda kwenye masoko.

Alisema baadhi ya wanunuzi wa zao hilo huwa wanaishia katika Mji wa Mbalizi hasa kipindi cha mvua wakiepuka kuongezeka kwa gharama endapo magari yao yatakwama kwenye maeneo ya vijijini ambako ndiko zao hilo linalimwa.

Mgombea huyo alisema kwenye Ilani ya CHADEMA, kuna utaratibu wa kuruhusu wakulima kuuza mazao yao mahali popote wanapoona wao kuna soko na kwamba ambao hawatakuwa na uwezo wa kusafirisha, watawezeshwa kuyafikia masoko hayo.





# Balozi Iddi aona mwanga huduma za afya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika hospitali mbalimbali nchini ni mwanzo mwema wa Zanzibar kujikomboa katika utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Balozi Seif Ali Iddi aliyasema hayo wakati akiukabidhi uongozi wa Hospitali ya Abdulla Mzee mkoani Pemba mashine ya kupimia damu kwa uchunguzi wa maradhi ya moyo, figo na ini pamoja na vitakasa mikono vilivyotolewa na mfanyabiashara maarufu Zanzibar, Said Nasser Bopar.

Alisema mfumo uliokuwa ukitumika wa baadhi ya wagonjwa kuwasafirisha kwenda Tanzania Bara na wengine nje ya nchi, mbali ya kutumia gharama kubwa, pia ulikuwa ukihatarisha afya za wagonjwa wanaosafirishwa wakati tayari wanasumbuliwa na maradhi.

Alisema serikali itaendelea kuongeza vifaa tiba ili kwenda sambamba na sera ya afya inayoelekeza kwamba huduma za afya ziwafikie wananchi wote tena, kwa wakati mahali popote pale mijini na vijijini.

Alimpongeza mfanyabiashara huyo kwa uzalendo wake anaoendelea kuufanya wa kuunga mkono sekta za elimu na afya.

Balozi Iddi alisema ni vyema vifaa vinavyotolewa kwa ajili ya huduma za wananchi vikaangaliwa vyema ili vitumike kwa kipindi kirefu.

Aliwataka watendaji wa afya, hasa madaktari, kuzingatia wajibu wao wa kusimamia sera ya matibabu bure iliyoasisiwa na Chama cha Afro Shiray Party baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1964.

Alisema haipendezi kuona baadhi ya watendaji hao wanatumia lugha ya ulaghai dhidi ya wagonjwa ambao wana haki ya kupatiwa matibabu bure kama ilivyoainishwa kwenye sera ya afya na miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali.

Balozi Iddi alisema katika kuhakikisha huduma za afya zinaimarika vyema na kuwafikia wananchi, haki za madaktari ikiwamo posho zao kutokana na kufanya kazi katika muda wa ziada, zinapatikana kwa wakati.

Alisema tatizo kama hilo ambalo pia limekuwa likiripotiwa kwa watendaji wa Hospitali ya Wete, lazima liondoke ili kutowavunja moyo watumishi hao.

"Mcheza kwao hutunzwa, hivyo tatizo hili lililokuwa kilio cha muda mrefu, lazima lipungue au kuondoka kabisa kwani inashangaza kuchukua karibu miezi sita, jambo lisilopendeza kabisa," aliagiza.

Akizungumza kwa niaba ya watendaji wa Hospitali ya Abdullah Mzee mkoani Pemba, Daktari Mkuu wa hospitali hiyo, Haji Mwita Haji, alisema kupatikana kwa mashine hiyo ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wanaofika kupata huduma za afya kutokana na maradhi mbalimbali yanayowasumbua.

Daktari huyo aliishauri serikali kuongeza uharaka wa ukamilishaji wa baadhi ya vifaa vilivyofungwa na vilivyo katika harakati za kufungwa.

Mfanyabiashara Said Nasser Bopar, alisema kuunga mkono sekta za elimu na afya ni dhima anayolazimika kuitekeleza katika kutoa huduma kwa jamii iliyomzunguka.




Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Hasina Omar, akizungumza na wadau wa uchaguzi katika kikao kilichofanyika Ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Maruhubi mjini Unguja jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa NEC, Ofisi ya Zanzibar, Hamidu Mwanga. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# NEC yaonya lugha chafu kampeni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Uchaguzi Tanzania (NEC), imevitaka vyama vya siasa na wagombea kuendelea kuzingatia maadili ya uchaguzi katika kampeni zao, ikiwamo kuepuka lugha za kashfa na maneno ya uchochezi yanayotishia usalama na amani ya nchi. Kamishna wa tume hiyo, Hasina Omar, alikumbusha suala hilo juzi alipofungua mkutano wa wadau wa uchaguzi uliofanyika kwenye Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) Maruhubi nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alivitaka vyama vya siasa na wagombea wake, kuepuka kufanya kampeni ambazo zinaashiria ubaguzi katika misingi ya jinsia, ulemavu, ukabila, udini, maumbile na rangi.

Kamishna huyo alivisisitiza vyama na wagombea kuwa kunapokuwa na malalamiko yoyote ya kimaadili, hatua stahiki zichukuliwe ikiwamo kuwasilisha malalamiko kwenye kamati ya maadili ndani ya muda uliowekwa.

"Wakati tume inaendelea kuratibu, kusimamia na kuendesha uchaguzi huu kwa kutumia sheria za uchaguzi, tunakumbusha wadau wetu wote katika kipindi hiki sheria nyingine za nchi hazijasimama, hivyo wajihadhari na vitendo ama matamshi ambayo yanaweza kusababisha vurugu kwa kisingizio cha uchaguzi," aliagiza. Alisema tume imejipanga kusimamia uchaguzi wa mwaka huu kwa kufuata katiba, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali na kila mdau akitimiza wajibu wake kwa kufuata taratibu, Watanzania watapiga kura kwa amani. Kamishna huyo alisema tume imeweka mazingira mazuri kwa watu wenye ulemavu na makundi mengine yanayohitaji usaidizi kupiga kura bila ya usumbufu.

Akiwasilisha mada kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwa wadau wa uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Kosmas Mwaisogwa, alisema daftari hivi sasa lina jumla ya wapigakura 29,188,347 ambapo 29,059,507 wako Tanzania Bara na 128,840 wako Tanzania Zanzibar.

Alisema ZEC imeandikisha wapigakura 566,352 ambao watashiriki kupiga kura ya kumchagua Rais na wabunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkurugenzi huyo alibainisha kwamba kati ya wapigakura 29,188,347 walioandikishwa, wanawake ni 14,691,743 na wanaume 14,496,604.

Alifafanua zaidi kuwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 35 ni 15,650,998, ambao ni wanaume 7,804,845 na wanawake 7,846,153.

Alisema kwa watu wenye ulemavu, jumla yao ni 13,211 wakiwamo 2,223 wenye ulemavu wa macho, 4,911 wenye ulemavu wa mikono na 6,077 wenye ulemavu wa aina nyingine.

Alisema NEC itatumia vituo vya kupigia kura 80,155 Oktoba 28. Kati yake vya Tanzania Bara ni 79,670 na Tanzania Zanzibar ni 1,412. Alisema tume imetoa vibali kwa asasi za kiraia 97 za ndani ya nchi kwa ajili ya kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka huu huku taasisi 17 za kimataifa nazo zikipatiwa vibali.

# TAMWA yaongeza nguvu vita ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, amewataka wadau wa mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia visiwani hapa kutokata tamaa ili kuifanya jamii kuwa salama.

Dk. Mzuri Issa Ali, alitoa rai hiyo juzi alipofungua mkutano wa wadau wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji visiwani hapa.

Alisema kila mmoja anawajibika katika masuala ya udhalilishaji katika jamii, hivyo msaada wa hali na mali unahitajika katika kufanikisha nguvu za mapambano hayo.

Alisema iwapo wanaharakati hawatapaza sauti zao katika kukemea vitendo hivyo, watoto na wanawake wataendelea kudhalilishwa na kufanyiwa ukatili.

Akiwasilisha mada kuhusu udhalilishaji, Asha Aboud kutoka Jumuiya ya Action Aid, alisema matukio ya udhalilishaji yanaendelea na kumekuwa na vikwazo vingi kuwatia hatiani walalamikiwa.

"Jamii kutokuwa tayari kutoa ushahidi, kuchelewa majibu ya vinasaba, kesi kuchukua muda mrefu, muhali, uchelewaji wa ufuatiliaji wa kesi pia ni kizingiti," alilalamika.

Washiriki wa mkutano huo walivitupia lawama vyombo vya sheria kwa kuchelewesha kesi za udhalilishaji na hivyo jamii kukata tamaa hasa kwa waathirika wa kesi hizo.

Akitoa ushuhuda, Asha Omar, ambaye mtoto wake wa miaka 13 alipewa ujauzito mwaka 2019, alisema tangu aliporipoti kesi hiyo, kumekuwa na ukimya mkubwa kwa vyombo vya sheria kujua hatua iliyofikiwa.

"Tangu mwanangu akiwa mjamzito mpaka sasa ameshajifungua, ninaambiwa subiri, utaitwa, tunafuatilia, ninasema kwa uchungu mkubwa kikao hiki leo kitanipa jibu sina imani na vyombo vya sheria." alilalamika.

Hakimu kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja ambaye alikuwa mwenyekiti wa mkutano huo, Shomari Omar, alisema ofisi hiyo kama mdau mkubwa wa sheria inasikitishwa na matukio ya udhalilishaji.

Aliitupia lawama jamii kwa kuendekeza muhali na kutokuwa tayari kutoa ushahidi pale wanapohitajika mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 - 269677.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe MWANGA WA JAMII

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 77 YA 2020**

**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu**

**MARY NGIWESAU LYIMO**

**NA**

**LILIAN THEODORE LYIMO..................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27 mwezi wa 10 mwaka 2020.
Hati hii imetolewa 09 Mwezi wa 10 Mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KIVUKONI
KINONDONI

115946102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI WILAYA DODOMA**

**MADAI NAMBARI 206/2020**

**MDAI HONEST DIONIS MASSAWE**

**MDAIWA MICHAEL SABOTA NYAMONGE**

**Kwa MICHAEL SABOTA NYAMONGE**
**BUNJU- DSM**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH 13,000,000/=.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku JUMATANO tarehe29/10/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiteta katika shauri hilo.
Na kama haukuhudhuria siku tajwa tajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo15/10/2020.

115945602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo SINZA**

**Usimamizi wa mirathi Na 253/2020**

**OMBI LA VINCENT EVARIST NJAU kuteuliwa msimamizi wa mirathi. Marehemu EVARIST BERNARD NJAU wa kajenge**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuudhuria kesi wakitaka mnamo Tarehe 30/11/2020 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 15/10/2020

Sahihi ya Hakimu

115946301

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo SINZA**

**Usimamizi wa mirathi Na 254/2020**

**OMBI LA VINCENT EVARIST NJAU kuteuliwa msimamizi wa mirathi. Marehemu ELIZABETH VUMILIA NJAU wa kidia.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuudhuria kesi wakitaka mnamo Tarehe 30/11/2020 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 15/10/2020

Sahihi ya Hakimu

115946301

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M. 1984 NYONGEZA )**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ARUSHA MJNI**

**Usimamizi wa mirathi Na 175 .... 2020**

**Ombi la ELINKIRA RODECK kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ELIZABETH RODECK KAMARA.**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA - BARA .**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10-11-2020 kabla huyo mwombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa . Tarehe 13-7-2020.

115945702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEYS HOTELS MOSHI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Landcruiser yenye namba za usajili **T 662 AAQ,** Yenye chassis namba **HJ750033838** na Injini namba **2H1182604** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**MOS/TR/RB/1166/2020**

115945102

## KUPOTELEWA NA LESENI YA PIKIPIKI

**MANYANDA SHIJA MANYANDA**
MKAZI WA MWANONO
DIDIA WILAYANI SHINYANGA,
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA
**LESENI YAKE YA PIKIPIKI,**
AMBAYO ILIPOTEA
MWEZI MEI MWAKA HUU .
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA
ATOE TAARIFA
**KITUO CHA POLISI**
KILICHOPO KARIBU
AU AWASILIANE NA
**MANYANDA SHIJA MANYANDA**
KWA SIMU NAMBA **0687807864.**
RB NAMBA
**SHY/RB/2020,**
CONTROL NAMBA
**9910819060331**

21594372

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
Katika mahakama ya mwanzo
**MJINI-MOROGORO.**
Usimamizi wa mirathi **No;303/2020**
Ombi la **JUMA SAIDI CHANDE** ,Kuteuliwa
msimamizi wa mirathi marehemu
**SAIDI SELEMANI CHANDE**
.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **06/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **tarehe 08/10/2020.**

21594492


***Uza,***

***Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# G20 yaongeza muda nchi maskini kulipa madeni

**RIYADH,** Saudi Arabia

MATAIFA ya kundi la G20 yamekubaliana kuongeza miezi sita ya ulipaji wa madeni kwa nchi maskini zilizokumbwa na janga la virusi vya corona.

Kundi la G20 limesema muda wa nyongeza uliokubaliwa juzi unaweza kuongezwa tena wakati wa majadiliano yatakayofanyika wakati wa majira ya kiangazi mwakani.

**Usimamishaji wa kulipa madeni ulikuwa unafikia mwisho mwezi ujao.**

Mkutano huo ulifanyika kwa njia ya video na kuhudhuriwa na mawaziri wa fedha na magavana wa kundi hilo.

Viongozi hao wameridhia kusogeza mbele hadi mwezi Juni mwakani kuwa muda wa mwisho kwa mataifa maskini kuanza tena kulipa madeni yake ili kuzisaidia nchi hizo kupambana na corona.

Usimamishaji wa kulipa madeni ulikuwa unafikia mwisho mwezi ujao.

Waziri wa Fedha wa Saudi Arabia, Mohammed al-Jadaan aliyekuwa mwenyeji wa mkutano huo alisema ingawa uchumi wa dunia unaimarika taratibu, mataifa maskini bado yanakabiliwa na hali mbaya kutokana na athari za corona. **DW**



Wanafunzi nchini Uganda wakiwa darasani huku wakiwa wamekaa umbali wa mita moja kwa ajili ya tahadhari ya maambukizi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: BBC**

## Uganda yaruhusu shule kufunguliwa

**KAMPALA,** Uganda

SERIKALI nchini Uganda jana imeruhusu shule kufunguliwa baada ya kufungwa kwa kipindi cha miezi saba kutokana na janga la virusi vya corona.

Walioruhusiwa kurejea shuleni ni watahiniwa wanaokamilisha masomo yao, huku shule na taasisi zikitakiwa kufuata kanuni za kudhibiti maambukizi ya corona.

Hata hivyo, shule kadhaa binafsi zinalalamikia kutosaidiwa na serikali kuweza kufadhili mahitaji ya wanafunzi kama vile vitakasa mikono na vipima joto, anasema mwandishi wa BBC Issac Mumena.

Mwezi uliopita, Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni, alitangaza kufunguliwa kwa shule kwa watahiniwa wa darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita, wanafunzi wa vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na biashara wanaomaliza mwaka wao wa mwisho kuanzia jana.

Shule hizo zinatakiwa kufunguliwa kwa kufauta masharti ya wataalamu wa afya ya kudhibiti corona.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya St. Daniel Yumbe iliyopo Kaskazini mwa Uganda, Aziku Mosese alisema wamejiandaa kwa ajili ya masomo.

Baadhi ya wanafunzi waliieleza BBC kuwa hawako tayari kuhudhuria masomo kwa sababu ya changamoto ya kushindwa kununua vifaa vya kujikinga na maambukizi ya corona kutokana na ukosefu wa fedha.

Shule zimefunguliwa nchini humo baada ya kulegezwa kwa masharti ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona. **BBC**

## Upinzani Ivory Coast wataka raia kupinga mihula mitatu

**ABIDJAN,** Ivory Coast

KAMPENI za uchaguzi mkuu nchini Ivory Coast zimeendelea jana huku upinzani ukitoa wito kwa raia kupinga azma ya Rais Alassane Ouattara, kugombea mihula mitatu.

Ivory Coast inatarajia kufanya uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwezi huu. Vyama vya upinzani vimetoa wito unaowataka ukaidi wa raia ili kupinga azma ya Rais Ouattara ya kugombea mihula mitatu huku wakitaja kuwa hatua hiyo ni kinyume cha sheria.

Jumamosi, maelfu ya watu waliandamana dhidi ya hatua hiyo katika mji wa kibiashara, Abidjan.

Kuna jumla ya wagombea wanne wanaowania kiti cha urais, ambapo wapinzani wakuu akiwamo Rais wa zamani na Waziri Mkuu wa zamani, walizuiwa kugombea baada ya kushindwa kutimiza vigezo vya uchaguzi.

Ouattara amekuwa Rais kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita katika uchaguzi ulioibua mgawanyiko na kukumbwa na ghasia. **BBC**

# 'Mashambulizi Idlib ni uhalifu'

**NEW YORK,** Marekani

SHIRIKA la Kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch (HRW) limesema katika ripoti yake kuwa mashambulizi ya ndege za Urusi na Syria dhidi ya raia katika Jimbo la Idlib huenda yakawa ni uhalifu dhidi ya binadamu.

Ripoti hiyo ya kurasa 167, iliyopewa kichwa cha 'Kulenga uhai Idlib,' iliandaliwa na shirika hilo baada ya mamia ya ushahidi wa picha na video za setilaiti kutolewa mwezi Aprili 2019 na Machi mwaka huu.

Mashambulizi hayo yaliwaua mamia ya raia na kuwalazimisha wengine zaidi ya milioni 1.4 kuyahama makazi yao.

Shirika hilo la kutetea haki za binadamu linasema kwamba mashambulizi hayo ambayo yanafanana na uhalifu wa kivita huenda yakawa ya uhalifu dhidi ya ubinadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Kenneth Roth alisema waliendesha uchunguzi wa mashambulizi 46 kwenye Mji wa Idlib ambayo yaliwalenga raia.

"Kwenye visa hivyo 46, wanajeshi wa Syria na Urusi walishambulia kwa makusudi taasisi au makazi ya kiraia. Yalilenga hospitali, shule, masoko na maeneo wanakoishi raia. Na siyo kwa bahati mbaya au walikuwa wakiwalenga wanaodhaniwa kuwa magaidi, bali kwa makusudi. "Hakukuwa na kambi yoyote ya kijeshi, adui yoyote, au kitu ambacho kingesababisha mashambulizi hayo dhidi ya taasisi za kiraia. Ni uhalifu wa kivita wa dhahiri."

Roth alisema lengo la kampeni hiyo ya kijeshi ya Urusi na Syria ya miezi 11, lilikuwa ni kuwafukuza raia na kugeuza maisha yao kuwa magumu ili vikosi hivyo kukalia maeneo hayo.

Serikali ya Urusi na Syria zimekanusha tuhuma hizo za kuwashambulia raia kwenye eneo ambako watu milioni tatu walikimbia makwao kutokana na vita ambavyo vimedumu takriban miaka 10.

Urusi inayounga mkono utawala wa Bachar el Assad, ilisema mashambulizi yao yamelenga makundi ya itikadi kali na yenye ushawishi kwenye eneo hilo.

Shirika la HRW lilisema serikali ya Urusi na Syria hazikutoa majibu kuhusu ripoti hiyo.

Operesheni ya kijeshi ya pamoja ya wanajeshi wa mataifa hayo mawili ilisitishwa baada ya kutiwa saini kwa mkataba wa usitishwaji mapigano baina ya Uturuki na Urusi.

Nchi hizo mbili zimekuwa kiunga mkono pande hasimu nchini Syria. **DW**

## Ujerumani yarekodi idadi kubwa corona

**BERLIN,** Ujerumani

ZAIDI ya watu 6,600 nchini Ujerumani wameripotiwa kupata maambukizi ya virusi vya corona ndani ya saa 24.

Idadi hiyo ni kubwa zaidi tangu ugonjwa huo uripotiwe nchini humo.

Hii inakuja saa chache baada ya Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, kusema kuwa hatua za kukaa nyumbani zitaimarishwa katika baadhi ya maeneo ili kuzuwia kusambaa kwa ugonjwa huo.

Hatua hizo ni pamoja na amri ya kutotoka nje wakati wa usiku na marufuku ya pombe na marufuku ya mikusanyiko ya umma. **BBC**



# DORTMUND KUTOMUUZA SANCHO JANUARI

**DORTMUND,** Ujerumani

KLABU ya Borussia Dortmund imemzuia Jadon Sancho kipindi cha madirisha yaliyopita ya usajili na hawana mpango wa kumuuza nyota huyo ifikapo Januari mwakani.

Sancho alikuwa akihusishwa sana na mpango wa kujiunga na Manchester United, lakini nyota huyo wa kimataifa wa England akabakia kwenye klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kama United wanapanga kumfuata wakati wa usajili wa Januari, inaonekana kwamba hawatafanikiwa.

Borussia Dortmund haitamuuza Sancho katika dirisha dogo la usajili, kwa mujibu wa gazeti la Bild.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, ameendelea kuhusishwa na United, huku Liverpool na Bayern Munich pia zimeonyesha nia ya kumtaka.

Mshambuliaji huyo alifunga bao moja na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi tatu za mashindano yote alizocheza msimu huu.



# Ronaldo amvulia kofia Neymar

**RIDO DE JAINERO,** Brazil

RONALDO Luis Nazario de Lima amepaza sauti kumsifia raia mwenzake, Neymar kwa kuivunja rekodi yake ya kufunga mabao mengi kwenye kikosi cha Brazil.

Neymar alifunga mabao matatu 'hat-trick' katika ushindi wa 4-2 kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Peru na kumfanya ampiku Ronaldo kwenye orodha ya wachezaji walioifungua mabao mengi Brazil.

Neymar alifikisha mabao 64 na kumpita Ronaldo mwenye mabao 62, akiwa amepitwa na Pele pekee mwenye mabao 77 katika rekodi ya mfungaji wa wakati wote wa timu hiyo.

Ronaldo, ambaye alishinda mara mbili Kombe la Dunia akiwa na Brazil kati ya mwaka 1994 na 2011, alitumia kurasa za mitandao ya kijamii kusifia mafanikio ya Neymar.

"Heshima zangu zote kwako wewe Neymar Jr!," aliandika Ronaldo mwenye umri wa miaka 44 kumzungumzia Neymar, juzi Jumatano.

"Anacheza sana, anatoa msaada, anacheza anapiga chenga na kusaidia timu. Hakika hongera kwake."

# Deschamps asifia uongozi wa Pogba

**ZAGREB,** Croatia

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amemsifia "uongozi" wa Paul Pogba baada ya kupata ushindi wa 2-1 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Croatia, juzi Jumatano.

Pogba alitokea benchi pale Zagreb na pasi yake ndefu ilimkuta, Lucas Digne aliyemtengenezea Kylian Mbappe aliyefunga bao la ushindi dakika ya 79.

Bao la uongozi la Antoine Griezmann dakika ya nane lilisawazishwa na Nikola Vlasic, lakini Ufaransa wakapata ushindi na kufikisha pointi 10 sawa na Ureno na kukaa kileleni kwa kundi A3.

Deschamps alimsifia sana kiungo huyo wa Manchester United, Pogba, hasa kwa pasi yake iliyofanya Mbappe kufunga bao la ushindi.

"Kuhusu Pogba, bila shaka tutamzungumzia yeye kuhusu kutokuwa na maswali kwa kiwango chake, lakini tunaweza kusema hivyo hivyo kwa Antoine Griezmann," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni mmoja wa viongozi, ana uwezo wa kufanya uamuzi na pia kuwa kiongozi wa kundi.

"Hakuanza kwa sababu ilikuwa ni busara kwake kutoanza, hasa kwa tatizo alilonalo.

"Lakini ndio ni mmoja wa wachezaji muhimu sana kwenye timu. Ingawa kuna wakati anaweza kuwa na wakati mgumu. Lakini bado ni mchezaji muhimu sana kwenye kikosi chetu."

Ufaransa itacheza na Finland kwenye mchezo wa kirafiki kabla ya kumaliza mechi za Kundi A3 dhidi ya Ureno na Sweden.



HABARI MICHEZO

# Southgate amtetea Maguire kwa kadi

**LONDON,** England

KOCHA wa England, Gareth Southgate amesema bado ana imani na Harry Maguire, baada ya mlinzi huyo kutolewa nje kwa kadi nyekundu wakati wakifungwa 1-0 na Sweden kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya Uefa, juzi Jumatano.

Nahodha huyo wa Manchester United, Maguire alionyeshwa kadi mbili za njano na kuwa nyekundu kwa kuwachezea vibaya, Yussuf Poulsen na Kasper Dolberg.

Christian Eriksen alifunga bao hilo pekee na kuipa ushindi huo muhimu Denmark katika mchezo huo.

Southgate alisifia kikosi chake kilichomaliza na wachezaji 10 uwanjani na kusema kwamba ni kundi lililoimarika.

Pia akamtetea Maguire mwenye umri wa miaka 27, kwamba alicheza vizuri na kilichotokea ni sehemu tu ya mchezo.

"Ni mchezaji mkubwa. Ana mchango mkubwa kwa kile tulichokifanya," alisema Southgate akiiambia Sky Sports.

"Kilichotokea ni sehemu ya mchezo, kwani hiyo sina wasiwasi naye, naamini ataendelea kuwa vizuri kwa michezo inayokuja."






# FERNANDES AKANUSHA KUMBWATUKIA SOLSKJAER

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amekanusha ripoti, kwamba alirushiana maneno na kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, wakati walipopoteza mchezo wa Ligi Kuu England, dhidi ya Tottenham.

Fernandes aliripotiwa kuwa na hasira alipotolewa nje wakati United ikiwa inaburuzwa kwa mabao 4-1, kabla ya kukumbana na kichapo cha magoli 6-1 pale katika dimba la Old Trafford.

Raia huyo wa Ureno alifunga bao la uongozi kwa penalti, lakini aliripotiwa kubwatukiana na Solskjaer wakati wa mapumziko.

Hata hivyo, Fernandes amekanusha taarifa hizo baada ya Ureno kuibuka na ushindi wa 3-0, dhidi ya Sweden kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa, juzi Jumatano.

"Kumekuwa na uvumi mwingine kuhusu hilo," alisema kiungo huyo akiiambia Sport TV.

"Mwanzo kulikuwa na majadiliano na mchezaji mwenzangu, Victor Lindelof, na baadaye Solskjaer.

"Naamini ilikuwa sehemu tu ya kuliimarisha kundi, na kile kinachozungumzwa sio cha kweli kabisa.

"Kipindi cha pili nilitolewa nje, na ni sababu za kiufundi tu na si vinginevyo. Kocha aliniambia aliona kama mchezo umeshaisha, kwani timu ilionekana haina tena uwezo wa kurudi mchezoni na kushinda."

# *Griezman: Deschamps anajua pakunichezesha*

**ZAGREB,** Croatia

ANTOINE Griezmann amesema Didier Deschamps anajua hasa wapi anapofiti yeye kucheza baada ya mshambuliaji huyo wa Barcelona kuwa na mchango mkubwa, wakati Ufaransa ikiibuka na ushindi, dhidi ya Croatia.

Griezmann alifunga bao la uongozi dakika ya nane, likiwa la tatu la kimataifa kwa mwaka 2020, wakati Les Bleus hao wakiibuka na ushindi wa magoli 2-1, pale mjini Zagreb.

Nyota huyo wa zamani wa Atletico Madrid alichezeshwa katika nafasi ya straika wa kati pamoja na Anthony Martial na Kylian Mbappe, ambaye alifunga bao la ushindi baada ya Nikola Vlasic kusawazisha.

Wakati aking'ara kwenye kikosi cha Ufaransa, Griezmann bado hajawa kwenye kiwango chake chini ya kocha mpya wa Barca, Ronald Koeman.

Akiwa anachezeshwa zaidi winga ya kulia, nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 ameshindwa kufunga au kutengeneza nafasi katika mechi tatu za LaLiga msimu huu wa 2020-21.

Hata hivyo, aliweka kando matatizo yaliyopo kwenye klabu yake na kurudisha kiwango chake na kuisaidia nchi yake kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mataifa ya Uefa, juzi Jumatano.

"Kocha anajua wapi kwa kuniweka mimi," alisema Griezmann akimzungumzia Deschamps katika mahojiano na TF1. "Inakuwa faida kwangu katika hali kama hii, kwa nafasi hii najiamini kwa kocha na wachezaji wenzangu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# COURTOIS AMTABIRIA MAKUBWA HAZARD

## Amwelezea kiungo huyo ana 'njaa' ya kuonyesha ubora wake katika kikosi hicho cha...

**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA, Thibaut Courtois amemtetea, Eden Hazard kwa kushindwa kutamba na kikosi cha Real Madrid baada ya kupata majeraha ya mara kwa mara.

**Hazard bado hajaichezea Madrid msimu huu, akiwa ameumia nyama za paja wakati akikaribia kurudi uwanjani.**

Kiungo huyo ameshindwa kuonyesha mchango wake kwa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu baada ya kutua hapo kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 100 kutoka Chelsea mwaka jana.

Lakini mchezaji mwenzake huyo wa Ubelgiji na Madrid, Courtois anaamini ni suala la muda tu kabla ya Hazard kuanza kuonyesha makali yake pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

"Hazard? Sina shaka nae, nina uhakika tutaona ubora wa Eden Hazard," amesema golikipa huyo akiambia Cadena SER, Jumatano.

"Ninamwona kwamba ana njaa ya kuonyesha kile alichonacho. Nina matumaini ataimarika haraka na kuwaonyesha watu kile alichonacho.

"Kabla ya majeruhi, alicheza mechi kadhaa vizuri na amekuwa na bahati mbaya ya kupata majeruhi ya mara kwa mara na hilo linamuumiza sana.

"Lakini mwezi huu nimemwona akijifua vizuri sana. Nina uhakika baada ya muda mfupi atakuwa vizuri na kuleta furaha kwa timu."

Courtois aliwasili hapo Madrid akitokea Chelsea mwaka 2018 na pia mwanzo alikuwa na wakati mgumu, lakini akarudi kwenye kiwango chake.

## ZISIKUPITE

### POGBA ANUKIA BARCA

KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 27, anataka kujiunga na Barcelona kwa uhamisho huru wa dirisha lilajo la majira ya joto. ***(Mundo Deportivo, via Sun)***

### OZIL AWAGOMEA WAARABU

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, 31, mapema mwezi huu alikataa ofa ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ili aondoke kwa washika bunduki hao na kutua katika Ligi ya Saudi Arabia (SPL). ***(Fabrizio Romano, via Express)***

### RUDIGER KUKOMAA CHELSEA

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 27, amesema anataka kurejesha nafasi yake ndani ya kikosi cha Chelsea baada ya uhamisho wake kukwama katika dirisha la usajili lililopita. ***(Athletic)***

### AGUERO AIKATAA INTER

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero, 32, hana mpango wa kuhamia Italia licha ya kusakwa na klabu ya Inter Milan. ***(Fabrizio Romano, via Sports Illustrated)***

### CHELSEA, JORGINHO KUTETA

CHELSEA wanajiandaa kuanza mazungumzo ya kuongeza mkataba na kiungo wa Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho, ambaye alihusishwa na mipango ya kuhamia Arsenal wakati wa dirisha la usajili lililopita. ***(AreaNapoli, via Express)***

### ALLEGRI ANUKIA UNITED

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano "Max" Allegri anaweza kuwania nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer, kama Manchester United itamtimua kazi kocha wake huyo. ***(Express)***

### SHAQIRI AIGANDA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Uswisi, Xherdan Shaqiri, 29, amesema aliamua kubaki kwenye klabu yake wakati wa usajili wa majira ya joto, licha ya kuhusishwa kutaka kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### COMAN HAKUTAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United haikuwasilisha ofa yoyote kwa ajili ya mshambuliaji wa Bayern Munich na Ufaransa, Kingsley Coman, 24, wakati wa dirisha la usajili, amesema mkurugenzi mtendaji wa klabu hiyo ya Ujerumani, Hasan Salihamidzic. ***(Bild, via Mail)***

### GRANT KUTUA WEST

WEST Brom imekubaliana ada ya uhamisho ya karibu pauni milioni 15 na Klabu ya Huddersfield kwa ajili ya uhamisho wa Karlan Grant, 23. ***(Sky Sports)***

### JUVENTUS, CITY VITANI

JUVENTUS imeungana na Manchester City katika mbio za kumwania mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, 28. ***(Sportmediaset, via Manchester Evening News)***

### LIVERPOOL KUMWACHIA WILSON

LIVERPOOL wako tayari kumwachia kwa mkopo, Harry Wilson, 23, lakini ilikataa ofa ya Swansea City kwa ajili ya winga huyo. ***(Athletic, via Wales Online)***

## Mayanja asubiri mkataba Ihefu FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Simba, Jackson Mayanja, amesema bado hajasaini mkataba na uongozi wa Ihefu FC, lakini amekiri kufanya mazungumzo na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mayanja ametoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa tetesi kwamba amesaini mkataba wa mwaka mmoja wa kukinoa kikosi cha timu hiyo ya jijini, Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayanja alisema kwa sasa yupo kwao Uganda, lakini klabu hiyo inakaribia kukamilisha mazungumzo ya kumwajiri kupitia kwa meneja wake.

Mayanja alisema mazungumzo yanaendelea vema na endapo mipango itakamilika, atarejea nchini kwa mara nyingine na kuiongoza timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu.

"Hizi taarifa za kusaini mkataba hazina ukweli wowote, sababu mimi niko Uganda ila kuna mtu wangu wa karibu aliniambia juu ya malengo ya uongozi wa timu hiyo, nipo tayari kurejea Tanzania," alisema Mayanja.

Taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema mabosi wa timu hiyo wanasubiri kauli ya mwisho ya mmiliki wa timu hiyo, ambaye kwa sasa yupo nje ya nchi na atakaporejea, atalimaliza suala hilo.

Ihefu ilitangaza kumfukuza kazi aliyekuwa kocha wake, Maka Andrew, ambaye aliipandisha timu hiyo baada ya kupata matokeo mabaya katika mechi tano zilizopita za ligi hiyo.

## Mgunda afunguka KMC 'iliwakamata'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema timu yake 'ilikamatika vilivyo' katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC, huku pia wachezaji wake wakishindwa kutumia vyema nafasi walizozipata.

Kauli hiyo ya Mgunda ilikuja baada ya kutoka sare ya bila ya kufungana huku timu yake pia ikikosa penalti baada ya kipa mkongwe wa KMC, Juma Kaseja kuipangua.

Mgunda alisema mchezo huo ulikuwa mzuri na timu yake ilitawala kwa kiasi kikubwa kuliko wapinzani wao, lakini tatizo la wachezaji wake lilikuwa ni umaliziaji mbovu.

"Tuliishika kabisa mechi, lakini utulivu wa wachezaji wangu kumalizia kufunga ndiyo ilikuwa tatizo, hivyo mimi kama mwalimu sichoki, siku zote mimi kwangu mwalimu wa mwalimu ni mechi, kwa hiyo mwalimu wangu wa mechi ya leo (juzi), amenionyesha mengi, nilichojifunza ni kwamba tunatengeneza nafasi nyingi, ambazo hatuzitumii," alisema Mgunda.

Katika mechi hiyo, Coastal Union italazimika kujilaumu yenyewe baada ya kukosa penalti dakika ya 43, huku pia wapinzani wao wakicheza pungufu katika kipindi chote cha pili kutokana na mchezaji wao, Ally Ramadhani kuonyeshwa kadi nyekundu.

# PENALTI YA KWANZA LIGI KUU BARA 'YAOTA MBAWA'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa katika raundi ya sita, penalti ya kwanza iliyotolewa kwenye mechi kati ya KMC FC dhidi ya Coastal Union ya jijini Tanga 'imeota mbawa'.

Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Coastal Union ilibahatika kupata penalti dakika ya 43, baada ya beki mmoja wa KMC kuushika mpira katika harakati za kuokoa, ikiwa ni penalti ya kwanza kupatikana msimu huu.

Hata hivyo, penalti hiyo iliyopigwa na Yusuph Soka iliokolewa kwa ustadi na kipa wa KMC, Juma Kaseja ambaye kwa miaka mingi anasifika kwa kuokoa mipira ya aina hiyo.

**Katika mechi hiyo, KMC na Coastal Union zilitoka sare, bila kufungana kwenye moja ya mechi za ligi.**

Msimu uliopita penalti ya kwanza ilipatikana kwenye raundi ya nne na mabingwa watetezi, Simba ndiyo iliyobahatika kuipata kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Kagera Sugar uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Septemba 26, mwaka jana.

Tofauti na penalti ya kwanza msimu huu kuokolewa na kipa, lakini hiyo ilitinga nyavuni, ikifungwa na straika wake hatari, Meddie Kagere dakika ya 78 ya mchezo, Simba ikishinda mchezo huo kwa mabao 3-0.

Azam FC yenye pointi 13 ndio inayoongoza katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 18 ikifuatiwa na Simba, Yanga, Biashara United ya Musoma na KMC wakati JKT Tanzania, Ihefu na Mbeya City zinaburuza mkia.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itaendelea tena leo kwa Dodoma Jiji FC kuwakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Jamhuri.




Mshambuliaji wa KMC FC, Reliant Lusajo (kushoto), akijipanga kumtoka mchezaji wa Coastal Union, Seif Yona katika mechi ya Ligi Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dirisha la usajili lafungwa Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), jana lilikamilisha mchakato wa usajili na uhamisho wa wachezaji kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohmmed Ameir, alisema mchakato huo umekuwa mwepesi kwa msimu huu, ikilinganishwa na msimu uliopita kwa sababu ya kuuendesha kwa mfumo tofauti.

Ameir alisema msimu huu timu zilijaza fomu zao kwa njia ya kompyuta wakati mwaka jana walitumia mfumo wa karatasi ambayo huitwa 'fomu mama'.

Alisema mchakato huo wa kupitia fomu za usajili ulihusisha timu 12 zitakazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar na nyingine 12 zitakazochuana kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja pamoja na baadhi ya timu, ambazo zipo katika ngazi za mikoa.

Alitaja changamoto kubwa iliyojitokeza katika usajili huo ni kubainika kwa baadhi ya wachezaji kuwa na mikataba na timu zao za awali, lakini kuomba kuhamishwa kwenda katika klabu mpya.

Kiongozi huyo alivitaka vilabu vyote kuwasilisha nakala za mikataba ya wachezaji wao, ili kuepuka matukio ya kusajiliwa na timu zaidi ya moja.


"Tunazipongeza klabu kwa kufanya mchakato wa usajili kuwa mwepesi, lakini tunawakumbusha kuwasilisha nakala za mikataba, hii itasaidia kubaini wachezaji ambao, wamezungumza na timu zaidi ya moja," aliongeza Ameir.

Wakati huo huo, ZFF kwa kushirikiana na Kamati ya Waamuzi Zanzibar, imefungua mafunzo ya waamuzi wanawake katika Mkoa wa Kusini Unguja na yatakuwa ya miezi mitatu.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 16, 2020

Nipashe

Courtois amtabiria makubwa Hazard UKURASA 22




Bondia Hassan Mwakinyo (mwenye miwani), akiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twisa (wa pili kulia), ambaye alikuwa anautambulisha mkanda wa mabara wa WBF ambao bondia huyo atautetea dhidi ya Jose Carlos Paz kutoka Argentina. Kulia ni bondia, Dulla Mbabe na kushoto ni Zulfa Macho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KAZE: NITAFANYA MAKUBWA YANGA

## ●●● Aahidi soka la burudani, kurejesha heshima lakini auweka 'kiporo' ubingwa Ligi Kuu...

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA mpya wa Yanga, Cedric Kaze, amewaambia mashabiki wa timu hiyo watarajie makubwa kutoka kwake, lakini Mrundi huyo akikataa kuwahakikishia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Kaze alitarajiwa kuwasili nchini jana usiku akitokea Canada ambapo alikuwa akipata mafunzo ya ukocha ya ngazi mbalimbali.**

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Kaze, alisema anaamini Yanga itapata mafanikio na kuwa 'tishio' endapo kutakuwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa wachezaji, viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Kaze alisema amejiandaa kukifanya kikosi cha Yanga kicheze mpira wa burudani na ushindani na anafahamu ni moja ya malengo yake kukabidhiwa mikoba ya kuifundishisha timu hiyo iliyoko kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Kocha huyo alisema anajua Yanga imesajili wachezaji wenye uwezo mkubwa kutoka mataifa mbalimbali na wanachohitaji ni kupewa mbinu mbadala za kusaka matokeo chanya katika mechi za mashindano mbalimbali watakazocheza.

"Siwahakikishii ubingwa, kitu ambacho ninawahakikishia mashabiki wa Yanga, watakuja kwenye mechi watafurahi, watatoka wanaimba na watasema kesho yake watakuja tena kuiangalia Yanga, tunaenda kufurahi," alisema Kaze.

Aliongeza bado hajasaini mkataba na Yanga, lakini ameshakamilisha mazungumzo ya kujiunga na klabu hiyo yenye makao makuu yake Mtaa wa Twiga na Jangwani.

Aliweka wazi ameshaiangalia Yanga katika mechi zake zote za msimu huu na baadhi za mwaka jana na kuona aina ya wachezaji waliopo, hivyo anafahamu mahali atakapoanzia kukijenga kikosi hicho.

"Nimeangalia mechi zote za ligi zile wamecheza, nimeangalia mechi zao za kirafiki, mechi walizocheza mwaka jana, naweza kusema nimepata mwanga wa wapi ninatakiwa kuanza, ninachowaambia Wana-Yanga, mimi na wachezaji wangu tutawapa burudani," Kaze aliongeza.

Kaze anatua nchini kuchukua mikoba iliyoachwa na Zlatko Krmpotic, ambaye alitimuliwa hivi karibuni baada ya timu hiyo kuonekana haichezi katika kiwango cha juu.

Awali Kaze ilipaswa atue nchini kuchukua mikoba ya Mbelgiji, Luc Eymael, lakini ilishindikana kwa madai ya kubanwa na matatizo ya kifamilia na hivyo Yanga ilimtangaza Zlatko aliyedumu kwa siku 37 kuwa kocha wake mpya.

Yanga ina pointi 13 baada ya kucheza mechi tano za Ligi Kuu Tanzania Bara, imeshinda mechi nne na kutoka sare moja, imefunga mabao saba imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara moja.

Mtihani wa kwanza wa Kaze utakuwa Oktoba 22, mwaka huu ambapo Yanga itaikaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

# Mwakinyo kuwania mikanda ya dunia

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

BONDIA bingwa wa mabara wa uzito wa Super welter, Hassan Mwakinyo anatarajia kupanda ulingoni kutetea mkanda wake wa Chama cha WBF katika pambano litakalofanyika Novemba 13, mwaka huu dhidi ya Jose Carlos Paz kutoka Argentina.

Mbali ya kutetea mkanda huo, Mwakinyo pia atawania ubingwa wa mabara wa uzito huo huo wa Chama cha IBA. Pambano hilo limepangwa kufanyika kwenye ukumbi wa Next Door Arena.

Mapambano hayo yamepewa jina la Dar Fight Night na yameandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Kelvin Twissa, alisema siku hiyo mabondia kutoka nchi tano watapanda ulingoni katika mapambano ya utangulizi akiwamo aliyekuwa bingwa wa dunia wa WBC, Fatuma Zarika kutoka Kenya ambaye atavaana na Patience Mastara wa Zimbabwe.

Twisa alisema bondia mwingine Mtanzania na mtoto wa kiungo wa zamani wa Simba, Zulfa Yusuph Macho atapigana na Alice Mbewe wa Zimbabwe wakati Abdallah Pazi maarufu Dullah Mbabe atacheza dhidi ya Alex Kabangu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alisema wameamua kuingia kwenye mchezo wa ngumi kutokana na kutambua vipaji vya mabondia mbalimbali hasa Mwakinyo ambaye anafanya vizuri katika mapambano yake.

"Tulifanya kazi na Mwakinyo kwa miaka mitatu na kuona ufanisi wake, tumeamua kuendelea naye na mabondia wengine wa Tanzania, tutaubadili mchezo wa ngumi nchini," Twissa alisema.

Naye Mwakinyo alisema ni fursa kwake na amejipanga kufanya vyema katika pambano hilo.

"Namshukuru Twissa na Kampuni ya Jackson Group Sports ambao wameonyesha nia ya kuubadili mchezo wa ngumi za kulipwa, sitawaangusha Watanzania," alisema Mwakinyo.

Mwakilishi wa WBF Tanzania, Chatta Michael alisema kuwa rais wa shirikisho hilo, Goldberg Howard ndiye atasimamia mapambano hayo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002